# Nipashe

Jumamosi Novemba 9, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580068

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mbunge Mwilima ajibiwa kuhusu mvuto ajira wafanyakazi ATCL

UKURASA 3




UKURASA 15

### UCHAGUZI MITAA:

# Serikali yatoa kauli Chadema kujitoa

**ACT** Wazalendo yafuata nyayo, Lugola ampa maagizo IGP Sirro waliofyeka shamba, mbunge kumtimua askari polisi...*Endelea ukurasa wa 2*

Distributed via ippmedia



## JPM AHIMIZA USHIRIKIANO KIUCHUMI AFRIKA, NORDIC

UKURASA 2

Rais John Magufuli, akisalimiana na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, baada ya kufungua Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi za Afrika na Nordic, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Rais mstaafu wa awamu ya pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Ahukumiwa kunyongwa kwa kuua mjukuu wake

UKURASA 3


**MICHEZO** STARS YASOGEZA MBELE CHALENJI YA WANAWAKE UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Serikali yatoa kauli Chadema kujitoa

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kutangaza kujitoa kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, Serikali imesema uchaguzi huo uko palepale na utafanyika siku uliopangwa.

Imesema vyombo vya ulinzi na usalama vimejipanga kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika katika hali ya amani na utulivu, huku ikiwaonya watu waliojipanga kufanya vurugu siku ya uchaguzi.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali (Tamisemi), Mwita Waitara, alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko (CCM).

"Kauli yetu ya serikali ni kwamba uchaguzi huu unaendelea kama kawaida, kama ilivyopangwa kwenye ratiba uchaguzi huo utafanyika Novemba 24, mwaka huu," alisema Waitara.

Naibu waziri huyo aliwaonya viongozi aliodai wanashiriki kuhamasisha fujo kupitia mitandao ya kijamii kuwa atakayebainika atachukuliwa hatua kali.

Katika swali lake, Monko alihoji: "Chadema wametangaza kujitoa katika uchaguzi na kuwakosesha wananchi haki yao ya msingi. Je, serikali ina kauli gani kutokana na kadhia hii?"

Akimjibu mbunge huyo, Waitara alisema suala la chama hicho kikuu cha upinzani nchini kujitoa katika kinyang'anyiro wamelisikia kupitia taarifa iliyotolewa na uongozi huo juzi.

Waitara alisema wananchi ambao wamejiandikisha na vyama ambavyo vipo kwenye mchakato viendelee na mchakato wa kushiriki katika uchaguzi huo.

"Lakini, itakumbukwa kwenye taratibu zetu ni kwamba wale waliokuwa na malalamiko, wameandika mapingamizi yao na kesho (leo) ndiyo siku ya mwisho na wao (Chadema) jana (juzi) walitoa tamko. Kwa hiyo, kama wamejiondoa, hawana sababu yoyote ya kulalamika kwamba hawakutendewa haki," Waitara alisema.

Aliongeza kuwa serikali inafanya kazi kwa karatasi kwa mawasiliano na haina nyaraka mezani, hivyo haiwezi kujadili jambo hilo.

"Rais ndiye mwenye mamlaka ya kutoa maelekezo nchi hii ya Tanzania, siyo kiongozi wa chama cha siasa. Sasa kiongozi wa chama cha siasa anatoa maelekezo kwenye chama chake na wanachama wake...," alisema Waitara.

Aliwaonya wakuu wa wilaya ambao wamekuwa na tabia ya kuhamasisha watu kuharibu mazao na kutishia watumishi wa umma kuwa watachukuliwa hatua.

"Tumepata taarifa kwenye mitandao kuwa wakuu wa wilaya wanaharibu mazao ya watu na kutishia watumishi wa umma, hivyo popote mlipo, kama kuna mtu anahisi hakutendewa haki kwenye uchaguzi huu na anafanya fujo mtaani sheria stahiki zichukue mkondo wake.

"Bunge halijawahi kutunga sheria inayosema ukigombea, ukanyimwa nafasi au ukahisi umenyimwa haki, ukafanye fujo ukigombea ukinyimwa haki au ukahisi umenyimwa haki, zipo taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa," alisema.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, pia alitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo, akisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama wakati wote wa kampeni hadi uchaguzi maeneo yote nchini.

Alisema jeshi hilo halitatoa mwanya kwa mtu yeyote kuvunja amani ama kufanya vitendo vinavyoweza kuashiria kuvunjika kwa amani.

"Jeshi la Polisi limejipanga wakati wote, kuanzia kampeni hadi siku ya uchaguzi, hakuna Mtanzania yeyote atakayefanya fujo ya kuzuru watu. Natoa onyo kwamba hakutakuwa na nafasi kwa chama chochote kitakachopanga kuvuruga amani, serikali tumejipanga kupambana na hali hiyo," alisema.

Waziri huyo alisema amemshamwelekeza Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, aanze kuchukua hatua kwa wahusika waliofyeka shamba la msimamizi wa uchaguzi wilayani Mbozi pamoja na mbunge aliyemtimua askari katika nyumba yake aliyopanga.

Jana, mmoja wa wabunge wa Chadema alidaiwa kumtimua askari polisi aliyekuwa amepanga kwenye nyumba yake na suala hilo kuhusishwa na hali ya kisiasa iliyopo nchini.

**ACT YAJITOA**

Siku moja baada ya Chadema kutangaza kujiondoa kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa, chama cha ACT-Wazalendo nacho kimetangaza kujiondoa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema wameamua kujiondoa baada ya asilimia 96 ya wagombea wake kuondolewa kwa sababu zisizo za msingi.

Zitto alisema uamuzi huo wa kujiondoa umetokana na kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho kilichofanyika juzi.

"Sisi tulikuwa na wagombea 173,000 lakini wameondolewa 166,000 sawa na asilimia 96. Kwa hiyo Kamati Kuu imeagiza hata hao asilimia nne walioachwa wajiondoe kushiriki kwa sababu bila kufanya hivyo tutakuwa tunahalalisha ubakaji wa demokrasia," alisemna Zitto.

"Tumejiondoa kwa sababu tumeondolewa, tusingejiondoa kihasara kwa sababu tulitumia nguvu kubwa kujiandaa. Watu wetu walijiwekeza kifedha kwa ajili ya kushiriki lakini wamekuja kuondolewa na watu ambao hawataki kushindana, wamebaka demokrasia," aliongeza.

Zitto alisema baada ya kujiondoa, Chama hicho kwa kushirikiana na vyama vingine vya upinzani, watafanya vikao na kujipanga kwa ajili ya hatua nyingine wanazopanga kuzichukua.

**Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (DODOMA) na Elizabeth**

Distributed via ioomedia



Mshitakiwa Ester Lyimo (41) akiwa chini ya ulinzi wa askari magereza, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua mjukuu wake Naomi John (7) kwa kipigo na kuhukumiwa kunyongwa mpaka kufa, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM asisitiza ushirikiano Nordic

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amezishukuru nchi za Nordic kwa uhusiano na ushirikiano wao mzuri na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania na kuzitaka kujielekeza zaidi katika ushirikiano wa kiuchumi.

Aliyasema hayo jana alipohutubia Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Afrika na Nordic uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Katika mkutano huo uliohudhuriwa na mawaziri 29 wa nchi za Afrika na watano Norway, Sweden, Denmark, Finland na Iceland, Rais Magufuli alisema Afrika inakumbuka mchango mkubwa uliotolewa na nchi za Nordic kabla na baada ya harakati za ukombozi.

Alisema katika mchango huo, nchi hizo zilichangia katika huduma za kijamii na kiuchumi kama vile afya, elimu, kilimo, sayansi na teknolojia, nishati, mazingira pamoja na kulinda amani na usalama.

Rais alitolea mfano wa Tanzania kutokana na nchi za Nordic kuchangia ujenzi wa Kituo cha Elimu Kibaha, Chuo cha Utafiti wa Kilimo Uyole, vyuo mbalimbali vya ufundi na kampeni za kufuta ujinga katika miaka ya 1970.

Hata hivyo, alisema kuna haja ya kubadilisha mwelekeo na kuingia katika mwelekeo wa kisiasa unaojikita katika ushirikiano wa kiuchumi kupitia biashara na uwekezaji.

Alisisitiza kuwa nchi za Nordic zenye watu wapatao milioni 27 zina uchumi mkubwa unaofikia pato la mwaka la Dola za Marekani trilioni 1.7 ikilinganishwa na nchi za Afrika zenye watu milioni 1.2 lakini pato la mwaka ni Dola za Marekani trilioni 2.334.

Kutokana na hali hiyo, alisema Afrika inapaswa kujifunza kutoka Nordic na amezikaribisha nchi hizo kuwekeza Afrika katika viwanda vitakavyoongeza thamani ya mazao, kuzalisha ajira na kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo.

Rais alibainisha kuwa Afrika ina fursa nyingi za uwekezaji ikiwamo eneo la ukubwa asilimia 30 ya eneo lote duniani linalofaa kwa kilimo, ukanda wa pwani ya bahari wenye urefu wa kilometa 30,500, mifugo, misitu, wanyamapori, mafuta, gesi, utalii na uchumi wake unaokua vizuri kwa wastani wa asilimia 4.1.

Pia alitoa wito kwa Afrika kujenga mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji kutoka nchi za Nordic na kusema kwa kutambua hilo, Serikali ya Tanzania imechukua hatua madhubuti za kuvutia uwekezaji huo ikiwamo kuwa na sheria za kuwalinda wawekezaji, kutekeleza mkakati wa kurekebisha na kuboresha mazingira ya biashara (The Blue Print) na kutenga kanda maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na uwekezaji.

Hatua zingine, kwa mujibu wa Rais, ni kujenga na kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kama vile barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, kujenga meli, kununua ndege na kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Bwawa la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 za umeme.

Baada ya kuhutubia mkutano huo, Rais Magufuli alifanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje wa Sweden, Ann Linde; Waziri wa Mambo ya Nje wa Norway, Ine Marie Eriksen Søreide na Waziri wa Mambo ya Nje wa Finland, Pekka Haavisto.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli aliwaomba mawaziri hao kupeleka salamu zake kwa wakuu wa nchi zao na amewahakikishia kuwa Tanzania iko tayari wakati wote kuendeleza na kukuza zaidi uhusiano uliopo, mkazo zaidi ukiwa katika biashara na uwekezaji.

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwa wameegesha baiskeli zao, kwenye mtaro wa maji ya mvua, katika Barabara ya Uhuru, mbele ya soko la Ilala Mchikichini, jijini humo jana na kwenda kwenye shughuli zao. Watu wengi wamekuwa wakiutumia mtaro huo sivyo na kuugeuza kuwa maegesho ya baiskeli na matoroli. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yamjibu mbunge mvuto wafanyakazi ATCL

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, amesema serikali haitumii kigezo cha mvuto katika kuajiri watumishi wa Shirika la Ndege (ATCL).

Nditiye alitoa kauli hiyo jana bungeni, baada ya Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Husna Mwilima, kusema juzi kuwa kuna haja shirika kuajiri wahudumu wenye mvuto.

Kabla ya kujibu maswali yaliyoelekezwa wizarani kwake bungeni jana, Nditiye alisema serikali na shirika hilo wameainisha sifa mbalimbali za kuajiri, ikiwa ni pamoja na kigezo cha kuwa Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18. Alivitaja vigezo vingine kuwa ni kuwa na ufahamu wa lugha za Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha na kuwa na cheti cha kuongoza ndege ama cha kufanya kazi ndani ya ndege. Nditiye alisema sifa nyingine za ziada ni kuwa na ufahamu na mambo mbalimbali ya kitaifa, kidunia na utalii. Alisema pia anatakiwa kuwa na hekima, heshima, maadili na huchunguza kama anafaa kuajiriwa.

Distributed via ipmedia

Mbunge wa Igalula, Mussa Ntimizi (CCM), alikuwa miongoni mwa wabunge waliouliza maswali yanayoihusu wizara hiyo, akitaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali ili wananchi wa jimbo lake wapate huduma ya mawasiliano ya simu.

Akijibu swali hilo, Nditiye alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano nchi nzima.

Alisema Julai mwaka huu, mfuko ulitangaza zabuni ya awamu ya nne kwa ajili ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata 521 zenye vijiji 1,222.

Alisema Kata ya Tura iliyoko katika jimbo la mbunge huyo, ilijumuishwa kwenye zabuni ikiwa na vijiji vya Karangasi, Mmunyu na Mwamlela na kwamba imeshafunguliwa na baada ya tathmini, mzabuni atapatikana katika maeneo hayo.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utaanza baada ya mkataba kutiwa saini mwezi ujao.

# Ahukumiwa kunyongwa mpaka kufa kumwua mjukuu kwa kipigo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imemhukumu Ester Lyimo (41), kunyongwa mpaka kufa baada ya kupatikana na hatia ya kumwua mjukuu wake Naomi John (7) kwa kipigo.

Lyimo ambaye wakati hukumu yake inasomwa kuanzia saa 8:18 mpaka saa 9:12, alisimama kizimbani macho makavu bila kuonyesha dalili za kusikitika wala kujutia tukio hilo.

Akisoma hukumu hiyo, Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Pamela Mazengo, aliyesikiliza kesi hiyo katika mahakama hiyo iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji, alisema bila kuacha shaka mahakama yake inamtia hatiani.

"Kama kungekuwa na adhabu nyingine zaidi katika mauaji ningeitoa hiyo. Mahakama yangu inakuhukumu kunyongwa mpaka kufa kwa kumwua Naomi kwa makusudi," alisema Msajili.

Alisema mahakama yake imezingatia wakati ushahidi wa Jamhuri unatolewa mahakamani, mshtakiwa alipoonyeshwa kielelezo namba moja ambacho ni picha tisa zilizoonyesha mwili wa marehemu ukiwa na majeraha mbalimbali mwilini na damu mpya kuvilia kwenye ubongo, mshtakiwa alijibu picha hizo ni za kawaida.

"Mshtakiwa ulipoonyeshwa picha za mwili wa marehemu zilizojaa majeraha ikiwamo sehemu za siri, hukujali, hukuonyesha kujutia wala kusikitikia kitendo hicho wakati wewe ndiye ulikuwa na jukumu la kumlea lakini ulimsababishia majeraha ukamwacha bila kumpeleka hospitalini kupata matibabu mpaka akafa," alisema Msajili Mazengo.

Alisema ushahidi wa Jamhuri bila kuacha shaka umethibitisha kosa la mauaji na umeungwa mkono na maelezo yake ya onyo mshtakiwa aliyokiri kumpiga mtoto huyo mara kwa mara.

Mazengo alisema sababu za kifo hazina ubishi kwamba ni kipigo kutoka kwa mshtakiwa ambaye alikuwapo eneo la tukio na kwamba ni wazi alikuwa na nia ovu.

Mapema mahakamani hapo, Daktari Msaidizi Mwandamizi, Modesta Lasana (52), alidai kwamba uchunguzi wa kifo cha Naomi ulionyesha kwamba alikufa kutokana na mivunjiko mwilini ikiwamo fuvu la kichwa kupasuka, damu kuvilia kwenye ubongo na majeraha yaliyotoa usaha.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Cecilia Mkonongo, shahidi alidai kuwa alikabidhiwa mwili wa Naomi aufanyie uchunguzi na kwamba kazi yake ina hatua mbili tofauti, ya kwanza nje ya mwili na pili ndani ya mwili.

"Nje ya mwili wa Naomi kulikuwa na makovu ya zamani na majeraha yaliyokuwa na vidonda vilivyotoa usaha ikiwamo sehemu zake za siri kuonyesha michubuko ya kitu kigumu,tumbo lilikuwa limesinyaa kwa kukosa chakula muda mrefu na makalio yalikuwa na vidonda vya kuunguzwa moto" alidai shahidi na kuongeza:

"Kwa upande wa ndani, kwa kuwa kichwa kilivimba nilifungua nikaona fuvu lilikuwa limekatika, damu mpya na ya zamani ilisambaa kwenye ubongo, mkono mmoja ulivunjika mara mbili na bega lilishuka."

Shahidi mwingine, Inspekta wa Polisi Salma Sechonge (43) alidai kuwa mshtakkwa alikiri

INAENDELEA UK. 8

# DCI ajivunia kwa kupungua uhalifu

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robart Boaz, amesema katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Jeshi la Polisi limefanikiwa kupunguza makosa makubwa ya uhalifu nchini.

Akizungumza na Nipashe juzi kuhusu mafanikio ya jeshi hilo katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, DCI Boaz alisema jeshi hilo pia limeongeza uwajibikaji.

"Utakumbuka wakati Rais John Magufuli anaingia madarakani, alipohutubia Bunge (Novemba 20, 2015) alitupa maneno mengi ambayo yalikuwa ni changamoto kwetu.

"Rais alisema angependa kuona uhalifu, hasa ujambazi, unatokomezwa, hakupenda kuona tena wananchi wanakuwa wanyonge na wenye hofu kwa sababu ya uhalifu.

"Ni kweli hakuna maendeleo pasipokuwa na amani, na sisi kwa kutambua hilo na kuzingatia kazi tuliyopewa na Rais, tulijipanga kuhakikisha tunafanya kazi kwa bidii kupambana na uhalifu huo," Boaz alisema.

Alieleza kuwa katika kipindi hicho cha miaka minne, Jeshi la Polisi limefaulu kudhibiti makosa makubwa ya uhalifu yaliyokuwa yanasumbua nchini, yakiwamo mauaji, ujambazi katika taasisi za fedha na uhalifu mwingine wa kutumia silaha.

Alibainisha kuwa kabla ya utawala wa serikali ya awamu ya tano, kuanzia mwaka 2011 hadi 2015, makosa makubwa ya uhalifu yalikuwa 327,935 wakati katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, makosa hayo yamepungua na kuwa na makosa 246,317.

Aliongeza kuwa mwaka 2011 hadi 2015, matukio ya mauaji yalikuwa 14,960 na katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, yamepungua hadi kufikia 1,097.

Kwa upande wa makosa ya usalama barabarani, alisema makosa makubwa katika eneo hilo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 yalikuwa 73,871 na miaka minne ya serikali ya awamu ya tano yamepungua na kuwa na makosa 22,621.

Boaz alisema makosa ya unyang`anyi wa kutumia silaha, mwaka 2011 hadi 2015 yalikuwa 4,515 na miaka minne ya utawala wa serikali ya

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# China yajitosa vita vya ujangili

**Na Lusungu Helela,** MIKUMI

UBALOZI wa China nchini, umeunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania katika mapambano dhidi ya ujangili kwa kuziwezesha jamii zinazoishi karibu na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi pembejeo za kilimo.

Pembejeo hizo zimetolewa kwa ajili ya kuzijengea jamii hizo uwezo wa kulima kisasa ili kuwasaidia kuacha kujihusisha na vitendo vya ujangili.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu alisema hayo jana wakati Ubalozi wa China nchini ukikabidhi msaada wa pembejeo hizo kwa wananchi wa kijiji cha Mhenda, Kilosa mkoani Morogoro.

Msaada huo ni mbegu za mahindi kilo 2,500, mbegu za alizeti 150 na mbegu za choroko kilo 800. Ubalozi huo pia umetoa jozi 13 za sare za ulinzi shirikishi, buti 13, komputa mpakato nne na runinga moja

Kanyasu alisema lengo la vifaa hivyo ni kuwasaidia wananchi kujikita katika kilimo cha kisasa kwa kutumia mbegu zenye ubora wa hali ya juu.

Akizungumza katika mkutano huo, Kanyasu alisema vifaa hivyo vitatumika katika kutoa elimu kwa wananchi katika mapambano dhidi ya ujangili.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliipongeza Jamhuri ya Watu wa China kukomesha soko la meno ya tembo na kuamua kutoa msaada kwa wanavijiji ili kuachana na biashara hiyo haramu.

Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke, alisema pembejeo za kilimo walizozitoa zitakwenda sambamba na mafunzo yatakayotolewa na wataalam kutoka China watakaowafundisha wanakijiji kulima kwa kisasa ili kuachana na ujangili.

Alisema Ubalozi wa China umeamua kuanza na kijiji hicho ili kuwasaidia wananchi kuzalisha mazao mengi ili wasiweze kujiingiza katika vitendo haramu.

Wang alisema China imeamua kuisaidia Tanzania katika vita dhidi ya ujangilli kwa vile watalii wanakuja nchini kwa ajili ya kuangalia wanyama, hivyo vitendo hivyo vinakwamisha juhudi za serikali katika kuleta maendeleo.

Naye Diwani Mhenda, Ali Athumani, alimshukuru Balozi wa China kwa msaada huo na kuahidi kuwa watakuwa mabalozi kwa vijiji vingine vilivyo karibu na hifadhi hiyo.

# Waliopopoa mawe msafara wa DC waiangukia serikali

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANANCHI wa Kijiji cha Mpunguti wilayani Kyela mkoani Mbeya, waliouvamia msafara wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta na kuushambulia kwa mawe, wameomba msamaha wakidai walifanya makosa na yanawagharimu.

Waliomba msamaha huo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya iliyokwenda kijijini huko kusikiliza kero za wananchi.

Baadhi ya wananchi hao wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kyela, Hunter Mwakifuna na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo, Ally Kinanasi, walilazimika kulala kwenye vumbi kuomba wasamehewe.

Mwakifuna alisema kutokana na kichapo walichokipata wananchi wa kijiji hicho kutoka kwa askari wa Jeshi la Polisi, baadhi walikimbia na mpaka sasa hawajarudi na hata walioko, wanaishi kwa wasiwasi wakihofu kukamatwa na polisi.

Alimwomba Mkuu wa Mkoa kuwasamehe wananchi hao kutokana na unyama walioufanya huku akidai kuwa kwa sasa wanashindwa hata kufanya shughuli za maendeleo kijijini huko kutokana na woga huo.

"Mkuu tunaomba utusamehe, tumekosa sana, ni kweli wananchi walipomvamia Mkuu wa Wilaya na wasaidizi wake, tulibaki hatuna namna maana ni kashfa ya aina yake kwetu, tunaomba tusamehe," Mwakifuna alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na tatizo hilo baadhi ya wazazi walitelekeza watoto wao, wakiwamo watoto 19 waliokuwa darasa la saba ambao walikuwa hatarini kutofanya mtihani, kama si jitihada za halmashauri ikishirikiana na viongozi wa dini na kijadi kuhakikisha hawakwami.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya

INAENDELEA UK. 8



Vijana wakiwa wanasafisha mifereji ya maji taka ili kuepusha magonjwa ya milipuko, katika eneo la Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lukuvi aagiza fukutwa mashamba pori 21

**Na Munir Shemweta,** KILOSA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameagiza mashamba 24 yaliyoko Kilosa mkoani Morogoro kupelekewa ilani ya kufutwa kutokana na kutoendelezwa.

Lukuvi alitoa agizo hilo jana wilayani hapa alipozungumza na uongozi wa Wilaya ya Kilosa na watendaji wa ardhi katika wilaya hiyo akiwa katika mwendelezo wa ziara ya kutatua migogoro ya ardhi mkoani Morogoro.

Alisema Kilosa haina kumbukumbu za mashamba jambo lililosababisha wizara kuamua kufanya upekekuzi maalum wa mashamba yote katika wilaya hiyo na kubaini mashamba 24 yasiyoendelezwa tofauti na mashamba 48 yaliyopendekezwa kufutwa awali.

Kutokana na agizo hilo, Wilaya ya Kilosa itakuwa na mashamba 72 yanayotakiwa kufutwa baada ya mashamba 48 ya awali kupendekezwa kutokana na kutoendelezwa.

"Maofisa Ardhi wa Wilaya ya Kilosa mfanye upekuzi wa mashamba yote yasiyoendelezwa bila upendeleo wala kumwangalia mtu usoni na wala msitishwe na mtu yeyote kwa cheo chake au utajiri wakati wa kufanya kazi hiyo," alisema Lukuvi.

Waziri Lukuvi alisema lengo la serikali kufuta mashamba yasiyoendelezwa ni kuwafikiria wananchi wanyonge wasio na ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo na kubainisha kuwa mashamba yatakatayofutwa yatagawiwa kwa wananchi na mengine yatatumika kama ardhi ya akiba itakayotumika kwa uwekezaji.

Aidha, Lukuvi alikemea tabia ya baadhi ya wananchi wa wilaya ya Kilosa kuuza au kukodisha mashamba wanayopatiwa na serikali na kusisitiza kuwa katika kukomesha tabia hiyo, wizara inaangalia namna ya kugawa mashamba yaliyofutwa kwa vikundi na kwa wale watakaopatiwa hawataruhusiwa kuuza.

"Mkuu wa Wilaya komesha tabia ya udalali wa mashamba unaofanywa na baadhi ya wananchi wa Kilosa na yale mashamba yanayogawiwa kwa wananchi yatumike kwa shughuli zilizokusudiwa," alisema Lukuvi.

Katika hatua nyingine, Waziri Lukuvi aliagiza wafugaji wote wanaomiliki maeneo yenye hati kuweka uzio ili kuepuka mifugo yao kwenda maeneo ya wakulima na kusisitiza kufanyika ufugaji wa kisasa.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoyi, aliomba kufanyika ukaguzi wa ardhi za vijiji kwa kuwa baadhi yake watu wamejimilikisha, wameuza na mengine kufanyika mgawanyo usio sahihi.

Kwa mujibu wa Mgoyi, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imeshindwa kufanya uhakiki kutokana na kutokuwa na fedha jambo alilolieleza kuwa limechangia migogoro ya ardhi na kusisitiza kuwa tegemeo la wilaya kwa sasa ni mashamba yaliyofutwa pekee.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, akizungumza na mafundi wa mikoa 10 ya kihuduma ya mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Na kuwataka kushughulikia changamoto za wateja kwa wakati ili kupunguza malalamiko na kuongeza ufanisi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe akana kutuma mawakala kuandamana

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, katika siku yake ya tatu ya utetezi, amekana mahakamani kutoa maelekezo kwa mawakala wa chama chake kufanya maandamano kwenda ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kufuata nakala za barua za utambulisho.

Kadhalika amedai kuwa hamchukii Rais John Magufuli bali anamshangaa.

Mbowe alieleza hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Hakumu Mkazi Mkuu Thomas Simba, wakati akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Joseph Pande, kuhusu kuwaagiza mawakala wake kufanya maandamano kwenda kwa Mkurugenzi.

Alidai kuwa siku ya tukio wakati wanamaliza mkutano wa kampeni, mawakala wa chama chake walikuwa hawajapata barua za utambulisho, hivyo aliwataka wafuatilie kwa amani.

"Niliwataka mawakala wafuatilie barua hizo sijui kama walitii au hawakutii kwa sababu walikuwa na taharuki kwa kukosa vitambulisho hivyo," alidai Mbowe.

Wakati akihojiwa na wakili wa serikali Jacqueline Nyantori, Mbowe alidai hakuwapo wakati wa matukio ya kifo cha Mwangozi, msaidizi wake Ben Sanane na aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki Tundu Lissu bali alisikia kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii ikiwemo JamiiFolam.

Alidai Jamiifolam si chombo cha uchunguzi na hakuwahi kuthibitisha taarifa hizo kama vyombo vya ulinzi na usalama vilihusika katika matukio hayo.

Mbowe pia alidai katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Kinondoni, chama chake kilishiriki na kilitia saini mwongozo wa maadili ya uchaguzi wa mwaka 2015 na ni sahihi mwongozo huo unaeleza namna ya vyama vya siasa kukosoana.

Alidai Februari 16, 2018 Chadema ilihitimisha kampeni za uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kinondoni katika Kiwanja Cha Buibui Mwananyamala na polisi ni miongoni mwa watu waliokuwapo katika mkutano huo.

Wakati akihojiwa na Wakili wa Serikali Salim Msemo, Mbowe aliieleza mahakama kuwa Jeshi la polisi ndilo linahusika na masuala ya kiupelelezi na hafahamu kama kuna idara ya upelelezi katika jeshi hilo.

Alidai kuwa wakati akitoa ushahidi wake mahakamani moja ya kesi alizotaja ni kuhusu kifo cha Mwandishi wa Habari Daudi Mwangosi na anaamini upelelezi wa shauri hilo ulifanywa na jeshi la polisi.

Mbowe alidai hana taarifa kama suala la kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wao wa hamasa Geita, Alphonce Mawazo, limeshafikishwa mahakamani na hoja za awali zilisomwa Agosti 28. mwaka huu.

Kesi hiyo imepangwa kuendelea mfululizo kuanzia Novemba 13 hadi 15, mwaka huu ambapo Mbowe ataendelea kuhojiwa na mawakili wa serikali.

Mbali na Mbowe washitakiwa wengine katika kesi hiyo ni Katibu Mkuu, Dk Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; na Mbunge wa Kawe Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washitakiwa wanakabiliwa na mashitaka 13 likiwamo la kula njama na kwamba wote wanadaiwa kuwa kati ya Februari 1 na 16, 2018, Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukuika tamko kutawanyika.

# Wanafunzi waonywa kuhusu siasa, ubaguzi

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI wa mwaka wa kwanza wa masomo 2019/20 wamefundwa na kutakiwa kuzingatia kilichowapeleka chuoni na si kujiingiza kwenye siasa na ubaguzi.

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kivukoni jijini Dar es Salaam, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa astashahada, stashahada na shahada waliojiunga na chuo hicho.

"Zingatieni kilichowaleta hapa chuoni. Mmekuja kusoma ili mfanye vizuri katika mitihani yenu, hivyo mjiepushe na vitendo vinavyoashiria ubaguzi na masuala ya kisiasa," alisema.

Prof. Mwakalila aliwataka wanafunzi hao wawe na nidhamu na kuwa na matumizi mazuri ya muda ili kufikia malengo waliyoyakusudia.


"Nimeamua kuzungumza nanyi kwanza kuwapongeza kwa kuchaguliwa katika chuo hiki cha Mwalimu Nyerer chenye historia iliyobeba jina la Mwasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere," alisema.

Prof. Mwakalila aliwaeleza wanafunzi hao kuwa pindi wanapokutana na changamoto wasisite kuziwasilisha kwenye uongozi wa chuo ili zitatuliwe.

Aliwakumbusha wanafunzi hao kuwa chuo hicho kilipoanzishwa kilikuwa kwa ajili ya kuandaa viongozi wazalendo ili waende kuongoza nchi.

"Mpo kwenye chuo ambacho kitawajenga kimaadili na uzalendo kwa ajili ya kuwa viongozi wazuri pindi mtakapotoka hapa," alisema.

Distributed via ippmedia



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Kilimanjaro, Zanzibar Queens Cecafa

**MASHINDANO** ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yanatarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 16 hadi 25 hapa jijini Dar es Salaam.

Michuano hiyo itashirikisha timu nane kutoka katika nchi wanachama wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati maarufu Cecafa.

Nchi hizo wanachama ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ni pamoja na wenyeji Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Zanzibar (Zanzibar Queens), Sudan Kusini, Burundi, Ethiopia, Kenya na Uganda.

Kwa maana hiyo, katika mashindano hayo ambayo hatua ya awali yamepangwa katika makundi mawili, Tanzania itawakilishwa na timu mbili (Kilimanjaro Queens na Zanzibar Queens).

Kama ilivyo kawaida, timu hizo mbili zinahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wadau wa soka nchini, kama ambavyo hufanya kwa kaka zao, Taifa Stars.

Mbali na kuwa wenyeji wa mashindano hayo, Kilimanjaro Queens, ndiyo timu pekee ambayo imeshinda kombe la michuano hiyo ambayo kwa mara ya kwanza ilianzishwa mwaka 2016, ikichezwa katika jiji la Jinja, Uganda.

Kilimanjaro Stars iliweza kushinda kombe hilo kwa kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza na ikafanikiwa kulitetea katika michuano mingine iliyofanyika mwaka jana jijini Kigali, Rwanda. Huu ni mwaka wa tatu na endapo wenyeji hao watafanikiwa kulichukua, itakuwa wanakibakisha jumla kikombe hicho hapa nchini.

Itakuwa si fahari au sifa kwa wachezaji, benchi la ufundi la Kilimanjaro Queens au wasimamizi wa mpira (Shirikisho la Soka Tanzania -TFF), itakuwa ni fahari kwa Watanzania wote na hasa wanamichezo kwa ujumla.

Kilimanjaro Queens na Zanzibar Queens, zinahitaji kupewa hamasa ya kiwango kile kile wanachopewa Taifa Stars, kwa sababu kazi wanayoifanya ya kupeperusha bendera ya Tanzania ni moja.

Zikiwa zimebakia siku chache kabla ya kuanza kwa mashindano hayo, yatakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, huu ndio wakati sahihi wa kuona wadau wataisadia timu hiyo na kuacha kusubiri kuwapa zawadi baada ya kulibakisha kombe hilo hapa nchini.

Ili wachezaji wafanye vizuri katika mashindano hayo, wanatakiwa kuandaliwa vema, kuiachia TFF peke yake jukumu la kuiandaa Kilimanjaro Queens na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kwa kuwaandaa Zanzibar Queens si jambo sahihi.

Kitendo cha kuwa wenyeji wa mashindano hayo kwa mara ya kwanza na kushinda kombe hilo mara mbili, tayari kila timu itakayoshuka dimbani itakuwa imejipanga kuhakikisha inapata matokeo mazuri dhidi ya Kilimanjaro Queens.

Hata hivyo, ili kuendeleza rekodi nzuri, Nipashe linawataka wachezaji na benchi la ufundi la Kilimanjaro Queens, kutobweteka na matokeo waliyopata katika mashindano yaliyopita, na badala yake kujipanga kuwakabili vema wapinzani wao na kulichukua tena kombe hilo.


Kama Kilimanjaro Queens imeweza, Zanzibar Queens pia wanaweza kupambana kuhakikisha wanafanya vema katika mechi zake na hatimaye ndugu hao wawili wakakutana fainali, na hapo tayari watakuwa wamejihakikishia kulibakiza kombe kwenye aridhi ya Tanzania.

Tunasema, hakuna kisichowezekana, kama timu ya vijana ya wanawake (Tanzanite), iliweza kuchukua ubingwa wa COSAFA ugenini Afrika Kusini, Kilimanjaro Queens na Zanzibar Queens, mnaweza pia kulibakisha kombe hili nyumbani kwa Rais John Pombe Magufuli.

Kila la heri Kilimanjaro Queens, Kila la heri, Zanzibar Queens.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ngoma ikivuma sana hupasuka

Na Barnabas Maro

**NGOMA** ivumayo sana kutokana na kupigwa huishia kupasuka. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote huharibika hasa linapopita kipimo chake.

Hapana shaka hivi ndivyo ilivyo kwa aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mkongomani Mwinyi Zahera kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambaye ana makazi yake nchini Ufaransa. Mkongomani huyu alikuwa anawatumikia "mabwana" watatu kila mmoja akipewa muda wake. Kuna wakati huwa na timu ya DR Congo kwenye michuano ya kimataifa. Pia huitembelea familia yake inayoishi Ufaransa na baada ya hapo huja kibaruani Dar es Salaam kuifunza Yanga.

Wahenga hawakukosea waliposema: "Mshika mbili moja humponyoka." Kwamba anayevishika vitu viwili lazima ataponyokwa na kimoja. Hutumiwa kumwelimisha mtu mwenye tamaa nyingi na kumkumbusha kuwa hawezi kufanikiwa katika yote ayatakayo.

Kadhalika walisema "Ngoma ikivuma sana hupasuka." Maana yake ngoma ivumayo sana kutokana na kupigwa huishia kupasuka. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote huharibika hasa linapopita kipimo chake.

Nani asiyejua au kukumbuka jinsi Zahera alivyopendwa na mashabiki na wanachama wa Yanga. Alikabidhiwa timu wakati Yanga ilipokuwa katika hali ngumu. Ilishindwa kusajili wachezaji wazuri na hata waliosajiliwa hawakupewa fedha za usajili.

Kwa sababu hiyo Yanga haikuwa na fedha; hivyo ikawa shida kupata wachezaji wazuri. Zahera alipambana na hali hiyo bila kuchoka kwa kuanzisha michango kutoka kwa wanachama na wapenzi wa timu hiyo.

Msimu uliopita timu ya Yanga pamoja na udhaifu wake wa hali na mali, iliweza kucheza mechi 10 bila kupoteza hata mmoja lakini ikafungwa na Mwadui ambayo pia ndio iliyovunja mwiko wa Simba kutofungwa msimu huu kwa kuifunga bao 1-0.

Mh! Mpira unadunda na ni mchezo wa bahati wasemavyo Waingereza kuwa "football is a game of chance." Timu yaweza kuitawala nyingine kwa muda mrefu mchezoni lakini kosa moja tu likatosha kubadili mwelekeo na kuwashangaza watazamaji!

Nadhani mapenzi ya wanachama na mashabiki wa Yanga yalimvimbisha kichwa Zahera kiasi kwamba yeye ndiye aliyekuwa kila kitu pale Yanga: kocha, msemaji, mchangishaji hela, na taratibu akawa mzungumzaji kuliko viongozi waliomsajili!Sijui mkataba wake ulivyo na kwa nini alisajiliwa ilhali ni kocha msaidizi wa timu ya nchi yake (DRC). Hii ilimpa nafasi ya kwenda kuitumikia timu ya nchi yake kila ilipokuwa kwenye michezo ya kimataifa.

Msimu huu ulipoanza, tena baada ya kusajiliwa wachezaji aliopendekeza, ghafla hali ikawa tata (mwendo wa polepole wa kumatamata kama wa mtoto anayejifunza kwenda; hali ya kutoeleweka). Ikawa hata wachezaji kutoelewana uwanjani!

Timu ilipotoa sare au kufungwa, Zahera alikuwa wa kwanza kulalamika na kwa kiasi kikubwa akiwatupia lawama wachezaji wake kwa "kutofuata maelekezo yake!"

Kadhalika alijitetea akisema baadhi ya viwanja havifai kwa mchezo wa kandanda. Ni kweli viwanja vingi humu nchini si vizuri lakini mbona timu zingine hushinda?

Sasa mahaba ya viongozi, wanachama na mashabiki hayapo kwa achezaji aliopendekeza wasajiliwe.

Kwa mfano anasema hakuona sababu wala umuhimu wa kusajili walinda milango watatu.

Kwa mara ya kwanza tangu alipotia saini mkataba wa kuitumikia Yanga, alirushiwa chupa za maji na makopo. Kama hiyo haitoshi, akatukanwa na mashabiki wa Yanga jijini Mwanza baada ya Pyramids ya Misri ilipowafunga mabao 2-1.

Ingawa baadhi ya watu walimshauri ajiuzulu, yeye aligoma katakata akisema hawezi kushurutishwa wala kufukuzwa na wanachama ila na viongozi. Pia akasema haogopi mkataba wake kuvunjwa. Akasema wanaoweza kuuvunja mkataba wake ni viongozi wa Yanga lakini apewe stahiki zake.

Hata hivyo alisema hana tatizo kabisa kuondoka Yanga na wala hana shaka na uamuzi wao lakini angesema hali aliyopambana nayo kwenye klabu ya Yanga hata kuwashangaza wanachama na mashabiki!

Mtu akimwona mwingine au wengine wanavunja sheria kisha akaamua kunyamaza, yeye pia anavunja sheria na anastahili lawama na kushtakiwa. Kwa nini sasa Zahera ndio yuko tayari kufichua mambo aliyokutana nayo akiwa Yanga mpaka wanachama na wapenzi wa klabu hiyo washangae?

Kwa nini hakusema wakati ule ili kuondoa sitafahamu (hali ya watu kutoafikiana kimawazo, kutoelewana au kusikizana juu ya jambo) katika klabu aliyokuwa akiitumikia ila anasema sasa baada ya kufukuzwa?

Wakati viongozi wakiwa kwenye hekaheka ya kupata mwalimu mwingine badala ya Zahera, aliyekuwa mchezaji na baadaye mwalimu wa Yanga, Charles Boniface Mkwasa ndiye aliyeteuliwa kufundisha timu hiyo kwa muda mfupi.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Kiwanda kikubwa mbolea kujengwa Lindi

**Na Zuwena Shame**

SERIKALI ya Ujerumani kwa kushirikiana na Denmark zinatarajia kuwekeza nchini kwa kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea mkoani Lindi chenye thamani ya Dola za Marekani bilioni tatu.

Msaidizi za Ubalozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Jörg Herrera, aliiambia Nipashe juzi kuwa serikali hizo ziko kwenye mazungumzo na Tanzania na hivi karibuni kiwanda hicho kitaanza ujenzi wake.

"Tumeanza mazungumzo haya miaka kadhaa iliyopita lakini tuna matumaini chanya kuwa yatamalizika hivi karibuni. Baada ya ujenzi kukamilika, tunatarajia kuwa si wakulima pekee watakaonufaika na mbolea za hali ya juu zitakazozalishwa lakini pia nchi inaweza kujipatia kipato kwa kuuza mbolea zake nchi zingine," alisema Herrera.

Aliongeza kuwa ujenzi wa kiwanda hicho utaleta ushawishi wa uanzishaji wa viwanda vingi zaidi mkoani humo hasa sehemu ambazo hazijaendelea kwa kuwa kutakuwa na upatikanaji wa ajira kwa watu wengi.

Herrera alisema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimekuwa kikisaidia uwezeshaji wa uwekezaji nchini na hata uboreshaji wa 'Blue Print' nchini kama hatua muhimu kulekea uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji.

Kuhusu uhusiano wa uchumi na biashara baina ya nchi hizo, Herrera alisema kuna idadi kubwa ya kampuni za Kijerumani nchini Tanzania kwa miaka mingi ama zenye ofisi au wawakilishi nchini na hii imeonyesha kampuni za kijerumani kuwekeza na kufanya biashara nchini.

Alisema kuwa katika kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Ujerumani, nchi hiyo imeanzisha ofisi ya biashara za nje ya Ujerumani (AHK) jijini Dar es Salaam.

"Si hayo tu, bali pia Ujerumani mara nyingi imekuwa ikileta nchini Tanzania jopo la wafanyabiashara na kuandaa mikutano ya kibiashara kwa serikali na wafanyabiashara binafsi. Mfano ni maonyesho ya kibiashara ya kimataifa ya na pia mwaka jana tulipata tuzo ya banda bora la kimataifa kwa miaka mitatu mfululizo" alisema.

Aliongeza kuwa japokuwa kumekuwa na changamoto za mazingira ya kibiashara miaka ya nyuma ikihusishwa na rushwa, serikali ya Tanzania imelitambua hilo na kulifanyia kazi, hivyo kuna matumaini chanya miaka ijayo.

Hata hivyo, aliongeza kuwa Ujerumani ina matumaini makubwa na soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Tanzania kuwa kitovu cha uingizaji biashara kwa kurahisisha na kuondoa msongamano wa bidhaa na watu mipakani.

Kuhusu uhusiano zaidi wa nchi hizo mbili, Herrera alisema kubwa wanaangalia nyuma na uhusiano madhubuti uliokuweao awali tangu kipindi cha ukoloni na mwisho wa karne ya 19 na pia kipindi cha vita uhusiano ulikuwapo katika nyanja mbalimbali.

Alisema uhusiano uliopo sasa ni mkubwa na wa ndani ambao kumekuwa na mawasiliano baina ya viongozi wa siasa akitolea mfano wa mazungumzo ya hivi karibuni kati ya Rais John Magufuli na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel kuhusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza baada ya Sala ya Ijumaa, kwenye Msikiti wa Nunge, Jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Mafia wachangamkia usajili simu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Wilaya ya Mafia na viunga vyake, wamejitokeza kwa wingi katika kampeni ya Mnada kwa Mnada kwa ajili ya kusajili laini za simu kwa kutumia kitambulisho cha taifa na kuhakikiwa na kampuni za simu.

Kwenye kampeni hiyo, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inashirikiana na kampuni za simu, Jeshi la Polisi Kitengo cha Uhalifu Mitandaoni, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Idara ya Uhamiaji.

Tangu kampeni hiyo ianze imekwenda katika mikoa 17 lengo kuu ikiwa ni kuifikia nchi nzima.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Mashariki, Mhandisi Lawi Odiero, alisema ni fursa kwa wananchi wa Mafia kufika katika uwanja wa Kilindoni kwa ajili ya kusajili laini zao kwa alama za vidole na kujiandikisha kupata usajili wa vitambulisho vya taifa kutokana na kuwa na mnyororo wadau wa mawasiliano.

Mhandisi Odiero alisema TCRA ilianzisha kampeni ya Mnada kwa Mnada ili kutoa fursa kwa wananchi kuhudumiwa hasa wakati huu usajili wa laini za simu kwa alama za vidole pamoja na huduma zingine za mawasiliano.

Aidha, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuimarisha ulinzi katika huduma za simu pamoja kufanya mawasiliano kuwa salama katika nchi. Alisema kampeni ya Mnada kwa Mnada ni kwa ajili ya kutoa elimu ya mawasiliano kwa kushirikiana na wadau katika kujibu changamoto wanazokutana nazo katika utumiaji wa mawasiliano nchini.

Mhandisi Odiero alisema wananchi wasio na vitambulisho vya Nida wahakikishe wanafika katika usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole na huduma nyinginezo za mawasiliano hayo.

Alisema kuna watu wengine wanatumia mawasiliano ya simu bila kujua ambapo Jeshi Polisi liko katika kampeni ya Mnada kwa Mnada ili kutoa elimu kuhusiana makosa ya jinai ya matumizi ya simu.

Mkuu huyo alisema kampeni hiyo ni endelevu katika kuwafikia ikiwa kuhakikisha kila mwananchi anajisajili laini yake kwa alama za vidole kwa kutumia kitambulisho cha taifa. Alisema TCRA iko kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi ili mtumie mawasiliano kwa usalama kutokana na elimu tunayotoa.

Hata hivyo, alisema kuwa wananchi wajitokeze katika kujisajili kwa alama za vidole kabla ya Desemba 31.

"TCRA tutahakikisha tunawafikia katika wananchi katika utoaji wa elimu za utumiaji wa bidhaa za mawasiliano kwa kutatua changamoto katika huduma hiyo," alisema.

# Mbinu kujiepusha magonjwa zatolewa

**Na Faustine Feliciane, MOSHI**

TAASISI ya Kilimo Hai Tanzania (TOAM), imesema magonjwa mengi yanayowakabili Watanzania tiba yake ya kwanza ni kutumia vyakula vya asili na kuachana na ulaji wa vyakula vya kemikali.

Taasisi hiyo imesema matumizi ya vyakula vinavyozalishwa kwa kemikali vingi vinachangia kuongeza magonjwa kama ya moyo na kansa.

Akizungumza kwenye semina ya wanahabari juu ya kilimo hai iliyofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro hivi karibuni, Mshauri wa Mawasiliano wa TOAM, Constantine Akittanda, alisema wakati umefika sasa kwa Watanzania kurudi kwenye ulimaji na utumiaji wa vyakula vya asili.

Mshauri huyo alisema miaka ya nyuma matatizo ya magonjwa yaliyopo sasa mengi hayakuwapo au yalikuwapo kwa kiwango kidogo.

"Jamii ni lazima ifike sehemu irudi nyuma kwenye kilimo chetu cha asili. Mazao yanayotokana na kilimo cha asili asilimia 100 yanakuwa hayana kemikali yenye sumu," alisema Akittanda.

Aidha, alisema hata kwenye soko la mazao, mazao yanayotokana na kilimo hai yanakuwa na bei kubwa sokoni kulinganisha na mazao ya kilimo cha kisasa.

"Nitolee mfano soko la zao la kahawa ya asili, Kahawa ambayo inalimwa kiasili sokoni imefika mpaka dola za Marekani 99 (zaidi ya Sh. 229,000) kwa kilo moja tofauti na kahawa ya kilimo cha kisasa bei yake iko chini zaidi," alisema.

Pia alisema iko mikakati ya Afrika ya miaka 50 ijayo ya kuhakikisha kilimo hai (kilimo endelevu) kinaendelezwa kwa nchi zote.

Kilimo hai kwa namna kubwa ni mkombozi wa wakulima katika kujipatia manufaa ya kazi yao kutokana na bei nzuri ya mazao yake.

# DCI ajivunia kwa kupungua uhalifu

INATOKA UK. 3

awamu ya tano yamepungua hadi kufikia 2,070.

"Kwa takwimu hizo tu, unaweza kuona kwamba amani imezidi kuongezeka katika kipindi hiki cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

"Haya ni mafanikio makubwa kwa maana kwamba wananchi wako huru zaidi kufanya shughuli zao kwa amani na utulivu, na sisi tunamshukuru sana Rais John Magufuli, amesaidia kutuongeza nguvu zaidi kwa kutujengea mazingira mazuri na ari ya kufanya kazi kwa bidii.

"Tutahakikisha kwamba matukio haya ya uhalifu yanazidi kupungua ili wananchi waendelee kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa kujiamini zaidi pasi na hofu ya kukumbana na wahalifu.

"Rais ametuwezesha kupata vitendea kazi vingi na vyenye ubora, makazi mazuri ya askari. Sasa, mfanyakazi akilala kwenye nyumba nzuri na familia yake iko mahali pazuri, ni lazima afanye kazi nzuri zaidi na ndiyo maana hata nidhamu yao kwa sasa imeongezeka sana.

"Hatusemi kwamba makosa haya yameisha kabisa, lakini sehemu kubwa ya askari, nidhamu yao imeimarika sana na hata kwa wachache ambao wanakosea, tumekuwa tukichukua hatua haraka sana kuwapeleka mahakamani na wengine kuwafukuza kazi kabisa," alisema.

Boaz alisema jeshi hilo liko katika utekelezaji wa mpango wake wa kupeleka askari kuanzia kwenye ngazi ya kata nchini.

"Kila kata itakuwa na askari wake ambaye atakuwa anaiongoza na lengo ni kutaka kuimarisha ulinzi kuanzia katika maeneo wanakoishi wananchi, na pia itasaidia zaidi kujua aina ya wananchi wanaoishi katika kata husika na kufichua zaidi wahalifu," alisema.

# Ahukumiwa kunyongwa mpaka kufa kumwua mjukuu

INATOKA UK. 3

kumpiga mjukuu wake Naomi John (7) (wakati wa uhai wake) mara kwa mara pamoja kumfinya sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kadhalika alidai kuwa alipomhoji mshtakiwa alikiri kurudia kumpiga na kumfinya sehemu zenye majeraha katika mwili wa Naomi. Shahidi mwingine, mtaalamu wa kupiga picha na kuchora ramani wa Jeshi la Polisi, Sajenti Mgeni (52), alidai kuwa alipewa kazi ya kupeleleza tukio la mauaji.

Alidai kuwa Machi 26, 2017 alipofika ofisini bosi wake alimkabidhi jalada la kupeleleza likiwa na watuhumiwa watatu wote wanawake, Ester Lyimo, Victoria John na Jacqueline.

Alidai kuwa kabla ya kuwahoji alimfahamisha bosi wake Mkuu wa Upelelezi wa Mbagala, Walelo, kwamba anataka kwenda eneo la tukio.

Shahidi huyo alidai kuwa aliongozana na askari wenzake Aloyce na mtoto wa mshtakiwa Victoria kwenda nyumbani kwake kwa sababu hawakupafahamu.

"Tulipofika tulipokelewa na watoto wawili wa kiume akiwamo Andrew ambaye alikuwa na mikwaruzo usoni, shingoni na mkononi nilianza kumhoji akanieleza majeraha hayo yametokana na kupigwa na mama mdogo. Nilipomfunua alikuwa anatisha zaidi ngozi ilikiwa ina majeraha kama kenge," alidai shahidi na kuongeza kuwa:

"Nilipomuona Andrew katika hali ile nikabaini kwamba walifanyiwa ukatili wa hali ya juu tofauti ni kwamba huyu mzima na yule amefariki, nilimpigia simu Afande Walelo akaniamuru nirudi kituoni na huyo mtoto."

Sechonge alidai kuwa alishuhudia jinsi Naomi (marehemu kwa sasa) alivyotumikishwa kazi za watu wakubwa tofauti na umri wake.

Alidai kuwa Mwanahamisi alijaribu kumsihi asiwapige lakini aliambua kununiwa, alipomsalimia hakuitikia na ikawa hawana mahusiano ya ujirani tena na kwamba alipomfikisha Andrew kituoni bosi wake alipomwona aliagiza apelekwe hospitalini na kwamba alilazwa.

"Machi 28, 2017niliungana na jopo la madaktari kufanya uchunguzi kwa kweli hali ya mwili wa marehemu ilisikitisha alikuwa na uvimbe mkubwa kichwani walipomfunua walibaini damu ilivilia kwenye ubongo, vidonda mwili mzima vilivyokosa matibabu na mkono wa kulia ulikuwa umevunjika" alidai shahidi huku akitokwa machozi ya uchungu.

Shahidi mwingine kutoka Dawati la Jinsia Polisi, Chang'ombe Koplo Joyce alidai kuwa siku ya tukio alipigiwa simu na Dk. Ruth anayehusika na ustawi wa jamii hospitali ya Temeke aende kuna tukio. Alidai kuwa alikwenda kitengo cha dharula akafahamishwa kwamba wamepokea mtoto lakini mshtakiwa na wenzake wanadai ni mgonjwa wakati tayari ameshafariki dunia.

Andrew John (9) alidai mahakamani katika kesi ya mauaji ya Naomi John (7) kwamba alimwona mama yake wa ubatizo, Ester Lyimo akimpiga mpwa wake mpaka akafariki dunia .

Andrew ambaye alikuwa akiishi nyumbani kwa mshtakiwa kwa sasa anaishi Moshi mkoani Kilimanjaro, mbali na kumwita mama wa ubatizo ni mama yake mdogo.

Dk.Abdukarimu Hasan (36) kutoka Hospitali ya Rufaa Temeke alidai kuwa siku ya tukio mshtakiwa aliongozana na watoto wake wawili huku akiwa amembeba mgongoni mtoto na mwingine mdogo wa miezi saba akiwa amembeba mkononi.

Alidai kuwa anamfahamu mshtakiwa alikwenda ofisini kwake na alipofika kitengo cha dharula kati ya saa 6:00 na saa 7:00 mchana alionyesha kupaniki na hofu na kwamba alijitambulisha amempeleja mjukuu wake anasumbuliwa na malaria.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Machi 25, 2017 Tuangoma Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam mshtakiwa alimwua mjukuu wake kwa kumpiga.



Wachuuzi wa madafu wakiyaandaa katika eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuingia mitaani kusaka wateja. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliopopoa mawe msafara wa DC waiangukia serikali

INATOKA UK. 4

Kyela, Ally Kinanasi, pia alimwomba Mkuu wa Mkoa kuwasamehe wananchi hao na ikiwezekana hata waliofungwa gerezani kwa kosa hilo nao waachiwe na kurejea kijijini kushiriki shughuli za maendeleo.

Alisema wananchi hao hawana hata uwezo wa kulipa gharama za uharibifu walioufanya kwenye magari ya serikali waliyoyapopoa mawe, hivyo akaomba wananchi hao wasamehewe.

"Sisi kama chama pia tunakuomba upite kwenye kauli ya Rais anayosema 'anaona huruma sana anapoona watu wapo gerezani', tunaomba utusamehe na ikikupendeza hata wenzetu walioko gerezani warejee," Kinanasi alisema.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwataka wananchi hao kuepuka kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa ni kosa la jinai na litawagharimu.

Alisema magari yote ya serikali ni mali ya wananchi kutokana na kwamba yanaendeshwa kwa kodi zao, hivyo kilichofanywa na wananchi hao ni kujiumiza na kujikosesha huduma.

Akijibu maombi ya wananchi hao, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema amewasamehe wananchi wa kijiji hicho, lakini hana mamlaka ya kuwatoa mahabusi gerezani, hivyo wasubiri uamuzi wa mahakama.

"Kitendo cha kurusha mawe kilinifanya nifikirie kuwa mlidhamiria kuua ama kuuawa, kitendo cha kumvamia askari mwenye bunduki, unataka akuue na mngeuawa, nisingetetea chochote," Chalamila alisema.

Alisema alimwagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa kupeleka askari 100 mara ya kwanza na baadaye akaagiza waongezwe hata 200 ili kuwatia adabu wananchi hao.



Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, Hamis Katimba (kushoto), akisoma taarifa ya utekelezaji wa miundombinu ya kituo kipya cha mabasi cha Makatanini, mjini humo, jana. Kulia ni Mkuu wa mkoa huo, Alexander Mnyeti. **PICHA: GIFT THADEY**

# JPM atoa mil. 152 ujenzi wa ofisi

Distributed via ippmedia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Mdhibiti Ubora wa Shule za Kanda ya Kaskazini Magharibi, Festus Stephano, amemshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa Sh. milioni 152 kwa kila halmashauri 100 nchini kwa ajili ya kujenga Ofisi za Mdhibiti ubora wa shule.

Aidha, shukrani za pekee alitoa kwa Rais kwa kufanikisha ujenzi wa ofisi nne za udhibiti ubora wa shule kwenye halmashauri nne za Mkoa wa Arusha. Akizungumza jana jijini hapa mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliyetembelea jengo la ofisi za mdhibiti ubora za shule za Jiji la Arusha na kulikagua, Stephano alisema jengo hilo na mengine matatu ya halmashauri zingine, yalianza kujengwa Juni, mwaka huu na kukamilika Oktoba.

Stephano alizitaja halmashauri zingine zilizojengwa ofisi hizo kuwa ni Karatu, Meru na Arusha DC na Arumeru.

Aidha alisema serikali pia imeahidi kutoa fedha zingine kwa ajili ya kujenga ofisi hizo kwa halmashauri za Monduli, Ngorongoro na Longido.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha shule zetu ambazo zinatoa elimu bure zinakuwa na ubora wa elimu wanayotoa kwa watoto wetu," alisema.

Naye Mhandisi Emmanuel Mshuza alisema jengo hilo lililoko kwenye Kata ya Moshono, limejengwa kwa fedha za serikali kuu kwa ajili ya kuhakikisha elimu bure inatolewa kwa viwango vya hali ya juu.

"Lakini eneo hili changamoto kubwa barabara kupitika wakati wa masika, japo tulipata wakati mgumu wakati wa ujenzi lakini tunamshukuru Mkuu wa Wilaya na Mkoa kutusaidia hadi tumekamilisha ujenzi huu,"alisema.

Gambo alisema kipaumbele cha kwanza cha serikali hii ni elimu na katika kutimiza azma hiyo, imekuwa ikitoa Sh. bilioni 1.9 kila mwezi kugharamia elimu bure kwa shule za msingi na sekondari.

Pia alisema kutokana na jitihada za serikali kuboresha elimu, mwaka huu Mkoa wa Arusha umeshika nafasi ya pili kitaifa katika matokeo ya darasa la saba.

"Nawapongeza walimu wote wa mkoa huu kwa kuwafundisha wanafunzi wetu vizuri na kushika nafasi hii. Lakini nawatahadharisha Mkoa wa Dar es Salaam ambao wameshika nafasi ya kwanza wakae chonjo," alisema.

# Viongozi wa dini wajipanga kutokomeza ukatili

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KAMATI ya viongozi wa dini mbalimbali wamejipanga kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto pamoja na vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi vinavyoweza kuzuilika.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mchungaji Niiteeli Panga wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kwenye kongamano la masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na afya ya uzazi, lililoandaliwa na Shirika la Misaada la Kanisa la Norway (NCA) mkoani Manyara

Alisema Kongamano hilo linawakutanisha viongozi kutoka Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata).

Mchungaji Panga alisema watu wanaoficha ukatili unaofanyika kwenye familia na jamii ni aibu kwa taifa.

"Viongozi wa dini na jamii husika wote tuna jukumu la kutokomeza vitendo vya kikatili. Lakini pia tukishirikiana na serikali na wadau wa maendeleo tunaweza kutokomeza tatizo hili," alisema na kuongeza:

"Inasikitisha tunaona mtoto anaumia sisi tunanyamaza kumbe ni aibu kuficha uovu huo. Watoto wetu wanakeketwa tunanyamaza hatuchukui hatua zozote," alisema Mchungaji Panga.

Kaimu Mkurugenzi wa Afya na Ustawi wa Jamii na Mjumbe wa Kamati ya Dini mbalimbali, Asina Shenduli, alisema NCA imeingia rasmi katika kupinga ukatili wa kijinsia na kila mwaka watakuwa na siku 15 za kupinga vitendo hivyo ambazo zitakuwa zinaanza Novemba 25.

Pia alisema kinachoshangaza katika afya ya uzazi ni mimba za utotoni zinazoendelea huku akitoa mfano wa utafiti uliofanyika hivi karibuni, unaonyesha kuwa Mkoa wa Katavi unaongoza kwa mimba hizo kwa asilimia 45 ukifuatiwa na Kagera asilimia 43 na Manyara asilimia 26.

Aliwataka viongozi wa dini na serikali kuchukua hatua, ili kunusuru watoto na mimba hizo, kwaajili ya kufanikisha ndoto zao zisikatishwe.

Ofisa Miradi wa NCA, Gwamaka Mwakyanjala, alisema viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika maendeleo na wanaweza kufanya mabadiliko panapohitajika.

Mwakyanjala alifafanua kuwa kuanzia mwakani, shirika hilo litakuwa na mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia ambao utakuwa mkubwa zaidi ya sasa.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto mkoani hapa, Emma Ngatoluwa, alisema ili kutokomeza vifo kwa kinamama vitokanavyo na uzazi, ni vizuri wajawazito wakaanza kuhudhuria kliniki wakiwa na mimba za miezi mitatu. Alisema kwa kufanya hivyo watapata ushauri wa kitaalamu na kuona maendeleo yao.

# RC ataka kuchunguza ubadhirifu wa fedha

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amemwagiza mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, kuchunguza fedha zinazolalamikiwa na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Magara kuwa zimeibwa.

Mnyeti alitoa agizo hilo juzi baada ya baadhi ya wananchi kulalamikia ufujaji wa fedha kwenye kijiji hicho unaodaiwa kufanywa na baadhi ya viongozi wa kijiji hicho.

Alimwagiza mkaguzi huyo wa ndani kuhakikisha taarifa ya uchunguzi huo itakapokamilika wananchi wanasomewa kwenye mkutano wa kijiji ili wajue kinachoendelea.

"Mnapofanya uchunguzi toeni na majibu kwa wananchi ili wabaini kilichofanyika kupitia mkutano wa kijiji si mnamaliza na kupeleka taarifa kwa mkurugenzi peke yake," alisema Mnyeti.

Alisema wananchi hao wanapaswa kujua kwenye ukaguzi huo endapo fedha zao zimefujwa au hesabu zipo sahihi hivyo wapewe mrejesho baada ya uchunguzi huo.

Awali, mkazi wa kijiji hicho, Juma Rajab, alilalamikia ufujaji wa fedha unaodaiwa kufanywa na baadhi ya viongozi wa kijiji hicho.

Rajab alisema alikamatwa na kulazwa mahabusu baada ya kuhoji matumizi ya ujenzi wa madarasa ya shule na manunuzi ya saruji na misumari.

Alisema aliuliza swali kwenye mkutano mkuu wa kijiji hicho ila yeye na wenzake watatu wakasingiziwa kuwa wanafanya vurugu kwenye kikao hicho ili hali walikuwa wanahoji haki yao.

"Nilikamatwa na kupigwa faini ya Sh.200,000 na sikupewa risiti viongozi wa CCM wa Kata ya Magara na Wilaya ya Babati waliingilia kati hadi nikaachiwa ila kuna ubadhirifu umefanyika," alisema Rajab.

Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Anastacy Bongwa, alisema wameshaanza uchunguzi wa miradi yote inayolalamikiwa na wananchi hao.

"Ukaguzi ukishafanyika tutakuja kuwapa wananchi majibu ya uchunguzi huo kwenye mkutano wa kijiji na wananchi watapata majibu yao kupitia malalamiko yao," alisema Bongwa.

Mnyeti yuko kwenye ziara ya maeneo mbalimbali ya mkoa huo ili kukagua na kuzindua miradi, kuzungumza nao, kusikiliza kero, changamoto zao na kuyapatia majawabu.

# Mafuriko yatishia hatma ya ushirika

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MAFURIKO katika bwawa la Nyumba ya Mungu na Mto Pangani yaliyotokea kipindi masika mwaka huu yamesababisha wakulima waliokopa mikopo kushindwa kurejesha fedha walizochukua kwenye taasisi za fedha.

Ilielezwa kuwa mafuriko hayo yalitokea wakati wa msimu wa masika kati ya Aprili na Mei, mwaka huu yamesababisha wakulima wengi waliokuwa wamekopa kwenye vyama vya ushirika wa akiba na mikopo na kuwekeza kwenye kilimo, kushindwa kurejesha mikopo hiyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Kaya, Elibariki Simbo, aliiambia Nipashe kuwa mafuriko hayo yamekiachia chama hicho jeraha kubwa kutoka na wanachama wake kushindwa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Wakati wa mafuriko hayo, wananchi wa Same waliokumbwa na adha hiyo walilazimika kuhama makazi yao na kuhifadhiwa katika kambi za muda za Rolesho, Bagamoyo na Marwa katika Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro.

"Mabadiliko ya tabia nchi ukiwamo ukame na maafa ya mafuriko ya mvua zilizonyesha katika Wilaya ya Same yamesababisa wakulima wengi waliokuwa wamekopa kwenye taasisi za fedha vikiwamo vyama vya ushirika wa akiba na mikopo na kuwekeza kwenye kilimo kushindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati,"alisema Simbo

Alisema pia uwepo wa wadudu waharibifu uliwafanya wakulika hao kushindwa kulipa mikopo hiyo ya zaidi ya Sh. milioni 200 na kukilazimisha chama hicho kuwaongezea muda wa kulipa.

Awali akizungumza kwenye mkutano mkuu wa 17 wa chama hicho, Meneja wa Kaya Saccos, Elvera Mdee, alisema kati ya Januari na Novemba mwaka huu, wametoa mikopo ya Sh. bilioni 1.2

"Pamoja na kwamba tumepiga hatua kubwa katika itoaji wa mikopo ya uwezeshaji kiuchumi, hatari nyingine ninayoiona kwamba kumeibuka tena wadudu waharibifu wa mazao maarufu kama kantangaze.

Mdee aliongeza: "Maana yake ni kwamba kama wadudu hawa wataendelea kuongezeka, wakulima wengi wanaweza kuchelewesha kurejesha mikopo yao kwa wakati kama ilivyotokea wakati wa mafuriko."

Akizindua tawi la chama hicho, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, aliwataka viongozi wake kufanya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo ujenzi wa majengo ya vitega uchumi, badala ya kutegemea riba na amana.

# DC atoboa viongozi walivyoziibia Saccos

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro Rosemary Senyamule, amewafichua viongozi 24 na mkakati wa siri wa kujikopesha bila kurejesha mikopo.

Alisema viongozi 24 wa vyama ushirika wa akiba na mikopo waliandaa mkakati huo wa kujinufaisha isivyo halali kwa kujikopesha mikopo pasipo kuirejesha. Kwa mujibu wa Semyamule viongozi hao ni kati ya wajumbe wa bodi za vyama 32 vilivyopo Wilaya ya Same.

"Nidokeze tu hapa kwamba kuna viongozi wa vyama 24 vya ushirika wa akiba na mikopo kati ya 32 vya Wilaya wanaotuhumiwa kujikopesha mikopo bila kuirejesha, na hivyo kusababisha vyama hivi kufa na vingine vikiwa katika hali mbaya zaidi,"alisema

Kutokana na tuhuma hizo, Senyamule alisema tayari hatua zimeanza kuchukuliwa dhidi ya viongozi hao ili kuhakikisha wanarejesha fedha hizo.

Kwa upande wake, Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Kilimanjaro, John Henjewele, alisema amependekeza kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini kuvifuta vyama hivyo katika orodha.

Alisema pendekezo hilo linalenga kubaki na vyama vichache vya ushirika wa akiba na mikopo ambavyo vina nguvu na ambavyo vinafanya vizuri katika tasnia ya ushirika.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Walimu, Omari Mchome , alisema wao kwa miaka 10 iliyopita, wametoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 15.9 kwa wanachama wake 1,500.

Mchome alieleza namna chama hicho kilivyobadili hali zao ya maisha, kwa kuwasaidia kujenga nyumba bora za kuishi, kusomesha watoto na kuanzisha miradi ya kiuchumi.

Aidha, katika taarifa yake, Meneja wa chama hicho cha walimu, Rosemary Kifunda, alisema wameanzisha utamaduni wa kukaa meza moja na wadaiwa sugu na kuweka upya mikataba ya kuirejesha kidogo kidogo.



Mfanyakazi wa shamba la Kahawa la APK, lililopo wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, akiandaa mbegu za miche ya kahawa ya kisasa kabla ya kuoteshwa katika vitalu vilivyopo katika shamba hilo jana. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Mhadhiri aonya nyuki kutoweka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MHADHIRI wa Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori cha Mweka, ameonya kuhusu kiwango kikubwa cha kutoweka kwa nyuki nchini.

Mwalimu huyo, Adolf Mremi, alisema kuwa iwapo hatua hazitachukuliwa kudhibiti shughuli za binadamu zinazoendelea hivi sasa ikiwamo uharibifu wa mazingira na matumizi makubwa ya dawa za kemikali, maelfu ya nyuki yataendelea kutoweka.

Mremi alisema matumizi ya kemikali katika mashamba makubwa ya kilimo na maeneo ya uwekezaji ambayo yanavutia nyuki kutua na kufanya kazi ya uchavushaji, yanaangamiza nyuki hao kila uchao.

Mhadhiri huyo aliyasema hayo jana katika Wilaya ya Moshi, wakati kikao cha wadau wa maliasili kilichopokea taarifa ya utafiti uliobaini aina mpya za nyuki 135 wanaopatikana nchini.

Alisema tafiti hiyo sasa itatumika kwa ajili ya kutoa elimu na kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu faida na umuhimu wa nyuki na kwamba aina kamili za nyuki waliopo nchini ni 3,000.


"Pamoja na kuwapo kwa mafanikio ya utafiti huo, shughuli za kibinadamu ukiwemo uharibifu wa mazingira na matumizi ya dawa za kemikali zinaangamiza maelfu ya nyuki na aina nyingine za wadudu. Ni lazima serikali ichukue hatua katika kunusuru nyuki hawa ambao ni utajiri mkubwa wa maliasili ya nchi yetu,"alisema Mremi

Ugunduzi wa aina hizo za nyuki, umefufua matumaini mapya ya Watanzania kuwa na aina ya kipekee ya wadudu ambao hawapatikani kwa wingi kiasi hicho katika ukanda wa Afrika.

Kwa sasa, utafiti wa aina hiyo unaendelea katika chuo hicho chenye wanafunzi kutoka nchi mbali mbali barani Afrika.

Aidha, mtaalamu wa nyuki kutoka chuo hicho, Julius Laswai, alisema pia wamegundua nyuki ambaye ana rangi ya blue anayepatikana katika eneo la Mlima Meru, uliopo chini ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

"Kunahitajika jitihada zaidi zimewekwa za kumlinda asihame kwenda mbali lakini pia kama taifa, hivi sasa Tanzania inapaswa kuhakikisha inakuwa na takwimu sahihi za nyuki waliopo, ingawa kuna taarifa kwamba wataalamu wanaendelea na kazi ya kupata takwimu sahihi,"alieleza mtaalam huyo





Mkurungenzi Msaidizi wa Magonjwa yasiyoambukiza katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Sarah Maongenzi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu wiki ya maadhimisho ya Kitaifa ya magonjwa yasiyoambukiza, itakayofanyika jijini humo, kuanzia leo hadi Novemba 14. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Distributed via ippmedia

# Waziri ahimiza matumizi wataalamu madini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza wachimbaji madini kuwatumia wataalamu kutoka Shirika la Madini la Taifa (Stamico) kupima maeneo ya miamba ya migodi kabla ya kuanza kuchimba badala ya kutumia ushirikina.

Aidha, serikali imesema imejipanga kutoa elimu ya uchimbaji madini, uchenjuaji na ujasiriamali kwa wachimbaji wadogo ili kuwapa namna ya kuhifadhi fedha zitokanazo na madini.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Madini, Stanislaus Nyongo, katika mdahalo wa uzinduaji sekta hiyo unaoendelea jijini hapa katika maadhimisho ya wiki ya Asasi za Kiraia (Azaki).

Nyongo alisema serikali imeamua kutoa wataalamu hao ili kuwasaidia wachimbaji kupata elimu kutokana na wengi wao kukosa maarifa juu ya uchimbaji na badala yake hutumia imani za kishirikiana katika uchimbaji jambo linasababisha kutumia nguvu nyingi bila mafanikio.

"Unakuta mchimbaji akifika mgodini anaweka mate mkononi halafu anayapiga kwa mikono miwili yanaporukia ndiyo anaenda kuchimba anadai mwamba uko upande huo," alisema Nyongo.

Kutokana na hilo alisema hivi sasa wanatoa wataalamu kwa wachimbaji ambao wanakwenda kuwapimia kwenye miamba kabla ya kuchimba na kuwaelekeza wapi madini yapo.

Nyongo pia alisema mchimbaji anakwenda kuuza nyumba, mwingine ng'ombe na kupeleka fedha migodini lakini anajikuta fedha yote imepotea na kufisilik kutokana na kutumia imani za kishirikina badala ya elimu ya kitaalamu kutoka Stamico.

"Kwa upande wa wachimbaji wakubwa haina shida, kazi iko kwa wachimbaji wadogo," alisema Nyongo.

Akizungumzia elimu ya ujasiriamali kwa wachimbaji, alisema ni suala muhimu sana kwa sababu wengi wao wamekuwa wakitumia fedha wanazozipata katika madini badala ya kuhifadhi kwa ajili ya kufanyia maendeleo.

"Tunaendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wachimbaji ili wahifadhi fedha hata pale wanapokosa madini wanakuwa na akiba," alisema Nyongo.

Kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika uchimbaji madini, aliwataka kutoa ushirikiano wakati wa ukaguzi, huku akiwasisitiza wanawake kuacha kukubali kutumika kwa miili yao kubeba madini kwa kuficha kutoka machimboni.

"Naomba niseme watu msikubali kuficha madini mpaka sehemu zisizo faa mfano madini ya Tanzanite katika mashine za kuscan hayatoi sauti hivyo wakijua unayo lazima wakukugue," alisema Nyongo.

# PM kuzindua mpango kudhibiti magonjwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kasimu Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza utakaofanyika leo jijini hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu Wiki ya Maadhimisho ya Magonjwa Yasiyoambukiza inayotarajiwa kufanyika kitaifa jijini kuanzia leo hadi Novemba 14, mwaka huu.

Alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na matukio mbalimbali yatakayofanyika ndani kwa kusimamiwa na Wizara ya Afya, maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na mkoa.

Miongoni mwa matukio hayo, kwa mujibu wa Dk. Mahenge, ni tamasha la michezo litakalokuwa na lengo la kuhimiza wananchi kufanya mazoezi ili kuzuia magonjwa yasiyoambukiza.

Alitaja tukio lingine kuwa ni upimaji wa afya ambapo kutakuwa na mabanda ya upimaji na matibabu ya magonjwa utakaoendeshwa na madaktari bingwa na watoa huduma wengine wa afya.

Pia alisema kutakuwa na tukio la kongamano la kisayansi litakaowakutanisha madaktari mbalimbali keshokutwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema katika kilele cha maadhimisho hayo, Waziri Mkuu anatarajiwa kutoa zawadi kwa washindi wa maadhimisho hayo na atamalizia kwa kuzindua mpango huo rasmi.

# Wabeba mizigo waonywa kutovaa vitambulisho

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wabeba mizigo katika masoko kuvaa sare ikiwamo vitambulisho ili kutambuliwa na wateja wanaowahudumia.

Agizo hilo limetolewa kutokana na kuwapo kwa wabeba mizigo wengi kwenye masoko ambao baadhi yao wamekuwa wakilalamikiwa kukosa uaminifu kwa kujihusisha na wizi.

Yuna alisema hayo katika kikao cha pamoja kati ya wabeba mizigo na uongozi wa jiji na kusema wabeba mizigo wamekuwa wakilalamikiwa na baadhi ya wateja wanaofika kupata mahitaji kwenye masoko.

Alisema kutokana na malalamiko hayo, ni muhimu sasa wavae sare na vitambulisho vitakavyowezesha kutambuliwa kwa wateja.

Sambamba na agizo hilo, ofisa huyo amewataka wabeba mizigo hao kushirikiana na uongozi wa soko, kuhakikisha watoto wenye umri chini ya umri wa miaka 18 hawajihusishi na ubebaji wa mizigo kwenye masoko.

"Kwa mujibu wa haki ya mtoto kamwe hairuhusiwi mtoto aliye chini ya miaka 18 kufanyishwa kazi," alisema.

Alisema ni wajibu wa kila mtu kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha ndani ya masoko watoto hao hawajihusishi na ubebaji mizigo.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii kata ya Majengo, Herielly Kutwama, aliwataka wabebaji hao kutumia lugha nzuri kwa wateja wanaowahudumia.

Pia aliwataka kupunguza unywaji wa pombe kwa kuwa kazi wanayofanyia ni sehemu ya ajira na inatakiwa kuheshiwa katika pande zote.

"Wamezidisha sana unywaji wa pombe na uvutaji wa bangi, hali hiyo imewasababishia walio wengi kupoteza mali za wateja na hàta na wao wenyewe kukosa nguvu" alisema.

Awali wabeba mizigo hao waliuomba uongozi wa soko kupandisha kiwango cha fedha wanazolipwa pindi wanapobeba na kushusha.

"Kiasi tunacholipwa cha Sh. 300 kwa ngunia ni kidogo, hivyo tunaiomba kipandishiwe hadi sh. 500 ili tuweze kukidhi maisha yetu" alisema mmoja wa wabeba mzigo hao, Halord Mathonya.






Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Simon Chacha akiwa ameketi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Minigo, wilayani humo, Mkoa wa Mara, mapema wiki hii, katika moja ya madawati yaliyotolewa na benki ya NMB, ili kusaidia kupunguza uhaba wa madawati shuleni hapo. Wa pili kushoto ni Kaimu Meneja wa benki hiyo Kanda ya Ziwa, Amos Mubusi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WFP yatakiwa kuwezesha dunia chakula, afya bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameitaka Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), liendelee kuihakikishia dunia mazingira yatakayowezesha kuwa na afya bora,

Aliyasema hayo Zanzibar wakati akiufungua mkutano maalum wa kimataifa uliowakutanisha Wawakilishi wa (WFP) wa Kanda ya Mataifa ya Kusini na Kaskazini mwa Afrika pamoja na Mashariki ya Kati.

Balozi Iddi alisema yapo mataifa mengi duniani yanaendelea kuwa na lishe duni inayosababishwa na wakimbizi kutokana na vita, ukame, mafuriko pamoja na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri mazingira.

Alitoa mfano wa matukio ya mabadiliko ya tabia nchi yaliyoikumba Afrika kwa mujibu waWFP mwaka 2018/2019, ambao umebainisha uwepo wa uzalishaji mdogo wa chakula katika sekta ya kilimo.

Alisema hitilafu hiyo iliyotokana na upungufu wa uzalishaji wa mazao umepelekea watoto wadogo kuwa na lishe duni inayoathiri maendeleo kutokana na upungufu wa chakula unaokumba zaidi ya watu milioni 220.

Akizungumzia uwajibikaji wa serikali kuimarisha ustawi wa lishe bora, Makamu wa Pili wa Rais alisema upo ushirikiano kati ya Tanzania na WFP kuimarisha lishe. Alisema WFP inaendelea kuiunga mkono Tanzania katika kuwapatia wananchi mafunzo ya elimu ya lishe bora, kusaidia moja kwa moja wakulima wadogo na huduma za usafiri kurahisisha mfumo wa mwelekeo wa kukua zaidi uchumi wa taifa.

Mwakilishi wa WFP Kanda ya Bara la Afrika Michael Danford, alisema shirika hilo limependekeza kuanzisha miradi mitatu Visiwani Zanzibar itakayosaidia kusukuma mbele masuala ya ustawi wa wananchi.

Danford alisema uamuzi huo wa shirika hilo umekuja kufuatia mchango mkubwa uliotolewa na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan wakati alipokuwa kiongozi wa ngazi ya juu ya shirika hilo miaka ya nyuma.

Distributed via ipnmedia

# Baraza lataka utalii kwa wote

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Kudumu ya Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, imeitaka Kamisheni ya Utalii kuzipatia elimu ya kutosha kamati za wilaya za utalii ili kufikia dhana nzima ya utalii kwa wote.

Akizungumza na Kamati za Wilaya za Utalii huko katika Ukumbi wa Wizara ya Habari Utalii na Mambo ya Kale Mjini Zanzibar Mwenyekiti wa kamati hiyo Mwantatu Mbaraka Khamis, alisema kamati hizo zikipatiwa elimu ya kutosha zitaweza kufanyakazi kwa ufanisi na kutekeleza vyema majukumu yao.

Alisema kumekuwa na changomoto mbalimbalii zinazoikumba dhana nzima ya utalii kwa wote hivyo ni vyema kamati hizo kupatiwa mafunzo na kuelimisha jamii ili kufikia lengo lililokusudiwa.

"Fursa hii ya elimu itaufanya utalii kwa wote kufaidisha wananchi wazawa kwani kamati zitaweza kufanya kazi kwa weledi na kutatua changamoto zilizopo", alieleza mwenyekiti huyo. Kwa upande wao wajumbe wa kamati za wilaya walisema zitafanya kazi kwa kuangalia maslahi ya Wazanzibari na serikali kwa ujumla ili kufikia dhana ya utalii kwa wote na si kuwanufaisha zaidi wageni na kuwasahau wazawa.

Aidha, waliomba kupatiwa ushirikiano na taasisi nyingine pamoja na wananchi ili kudhibiti biashara haramu katika fukwe, kulinda Mila, silka na Utamaduni wa Mzanzibari pamoja na maeneo ya kihistoria yasiharibiwe kwa lengo la kuongeza pato nchini.

Mapema Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii Abdallah Muhamed Juma, alisema kamati za kiwilaya zitashirikiana na kamisheni kwa ajili ya kusukuma mbele maendeleo ya utalii ndani ya wilaya.

Aidha, Katibu Mtendaji alisema kamati hizo zitakuwa na majukumu ya kuimarisha utalii kwa wote, kudhibiti usalama na amani kwa wageni na wenyeji wa maeneo ya utalii, kuazisha mfumo wa fedha wa jamii kwa kutoa asilimia moja ya pato la muekezaji ambazo zitatumika kwa maendeleo ya vijiji.

Alisema pia kamati hizo zitakuwa na jukumu la kulinda na kudumisha utamaduni za asili kama bidhaa ya utalii, kudhibiti thamani, maadili katika wilaya kudhibiti pamoja na kuunga mkono jumuiya za kiraia zinazofanya shughuli za utalii kwa kuzisaidia kwa kujishuhulisha katika mipango yao kwa kushirikiana na kamisheni na wadau wengine wa utalii.

# Ubunifu, teknolojia kuboresha elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR ina nafasi kubwa kukuza viwango vya elimu kupitia teknolojia mpya, iwapo wadau wa sekta ya elimu watakuwa wabunifu na kutumia kikamilifu fursa za utaalamu mpya utokanao na teknolojia hiyo.

Akifungua warsha iliyowakutanisha watendaji na wataalamu wa teknolojia kutoka taasisi mbalimbali za elimu , Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Simai Mohammed Said, alisema umefika wakati kuwahamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi na hesabati.

Warsha hiyo imeongozwa na wataalamu wa ufundishaji kwa njia ya roboti kutoka nchini Zimbabwe na Denmark sambamba na wakufunzi na wataalamu wa elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kutoka taasisi mbalimbali za kielimu na nyengine zinazohusiana na sekta hiyo Zanzibar. Said alisema, ili kuhakikisha azma ya Zanzibar na Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda inafanikiwa, hapana budi kutilia mkazo masomo ya sayansi na kuwashajiisha wanafunzi wasiyaogope na kuyakimbia.

Alieleza kuwa, kwa kutambua umuhimu wa kuwekeza kwenye masomo hayo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na sekta binafsi, imejizatiti kuimarisha miundonmbinu ya elimu ili kuhakikisha maendeleo yake yanaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani.

Alieleza kuwa, kutokana na umuhimu wa matumizi ya teknolojia kwa maendeleo endelevu, lazima wanafunzi wafunzwe kuwa wabunifu na kuonyesha vipaji vyao kwa manufaa yao na taifa kuelekea Tanzania ya viwanda. Alisema iko haja kutengeneza mazingira rafiki kwa kuwa sasa kunaibuka vijana wengi wenye uwezo na ujuzi wa kutumia mitandao ya kijamii lakini wanakosa fursa za kuwainua na hivyo kubaki wakiitumia kwa mambo yasiyofaa badala ya kukuza vipawa vya elimu yenye tija.

"Sisi viongozi wa kisiasa tunapoalikwa kwenye mikutano ya kikazi nje ya nchi, tunapaswa kutafuta fursa na misaada mbalimbali na inapopatikana ni juu ya watendaji wa ngazi mbalimbali kuandaa programu nzuri ili nchi iweze kunufaika na matunda hayo," alisema.


Mkurugenzi wa Idara ya Teknolojia na Mawasiliano katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Omar Said Ali, alisema lengo la warsha hiyo ni kuangalia jinsi mfumo wa kiroboti unavyoweza kutumiwa na kwa skuli za Zanzibar na kuongeza ubunifu na ufahamu wa masomo ya sayansi na hesabati.

Alisema warsha hiyo iliyopewa jina la 'Stem and Robotic' ambayo ni matunda ya Naibu Waziri kuhudhuria mkutano wa Umoja wa Afrika kuhusu kukuza elimu uliofanyika nchini Botswana Agosti 2019, ni mkakati maalumu kuhakikisha nchi za Afrika zinaongeza idadi ya watu wenye ujuzi stahiki wa kukuza fursa za ajira.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Abdullah Mzee Abdulla, alisema utaratibu huo ni muhimu katika kuzifanya nchi za Afrika kuwajenga walimu na wanafunzi katika kujitegemea kutokana na taaluma wanazozipata.

Alieleza kuwa, katika dunia ya sasa, elimu ya sayansi na teknolojia ndiyo inayopewa nafasi zaidi kuzalisha ajira katika viwanda na sekta ya ufundi, ambazo zinaweza kuimarisha uchumi wa mataifa na kuinua ustawi wa wananchi wao.


Sally Kim Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Edustore Afrika yenye makao makuu yake Afrika Kusini, pamoja na Meneja wa 'Shape Robotic' nchini Denmark . Shan Mari Linnet Nissen, walieleza kuwa, wadau wa sekta ya elimu wanapaswa kuonyesha ujuzi wao kwanza badala ya kusubiri fedha kutoka serikali zao.



**ODEMBA** Soma UK.14

JUMAMOSI NOVEMBA 9, 2019

BT
BURUDANI TELE



Distributed via ippmedia

# AMEJIKAZA KIUME

## JUX AKUBALI YAISHE

Soma UK.16

## BASI SAWA



## Nandy amnogesha Magufuli

REMIX ya wimbo wa Ninogeshe ambao mwanamuziki Nandy amemwimbia Rais John Magufuli umepokelewa vizuri na mashabiki.

Wimbo huo unaoitwa 'Magufuli' una siku nne tangu kuachiwa kwake lakini umepata watazamaji wengi katika mtandao wa Youtube

Wimbo huo unaelezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana tangu Rais Magufuli kuingia madarakani.



## Odemba awakumbuka wanafunzi Mkuranga

MWANAMITINDO wa Tanzania, Miriam Odemba, ametoa msaada wa kisima cha maji katika Shule ya Msingi Kiwambo, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

Akizungumza baada ya kukabidhi kisima hicho, Odemba amesema ameamua kutoa msaada huo baada ya kuona wanafunzi wanaosoma shule hiyo zaidi ya 300 wanapata tabu ya kupata maji safi na salama wakati wa masomo.

"Nimeguswa na wanafunzi hawa, nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza niliona wanafunzi jinsi wanavyohangaika kutafuta maji, hivyo kisima hiki kitasaidia kutatua kero hii," amesema Odemba.



# SETH APATA NAFUU AOMBA MSAADA

MAMA Kanumba amezungumzia hali ya mtoto wake Seth Bosco na kueleza ameanza kupata nafuu, lakini amewaomba Watanzania kumsaidia kupata bima ya afya.

Amesema kwa sasa miguu yake imeanza kupata fahamu tofauti na huko nyuma ambapo alikuwa hana hisia.

"Nawashukuru Watanzania kwa kumuombea kila siku ili apone, dua zao zimeanza kufanya kazi lakini kama mama naomba msaada wa bima ya afya ili kumudu matibabu yake," amesema mama Kanumba.

## INSTA-TWITTER





**Tunashukuru** kwa uwepo wako Papaa Zahera ndani Yanga African. Tutakukumbuka sana, kila la kheri uendako-**Flora Mvungi.**



**Mbwa** mwitu walimwandaa Daudi kukabiliana na simba pindi alipokuwa ni mchungaji wa kondoo katika familia ya Yesse. Simba nao wakamwandaa Daudi kukabiliana na mtu hatari Goliati. Vilevile, Goliati alimuandalia njia Daudi kukabiliana na Sauli. Na sauli akamuandaa Daudi kuchukua ufalme wa Israel. Mungu huruhusu hali fulani ngumu ili kukuandaa kuwa katika nafasi nzuri na kubarikiwa-**Mwijaku.**



## Hemed unataka kujenga kijiji chako?

MWIGIZAJI mkongwe na mwanamuziki Hemedy Suleiman 'PHD', ametangaza kusitisha mpango wake wa kugawa mbegu za kiume baada ya kuelemewa na idadi kubwa ya watoto.

Akizungumza na EATV na EA Radio Digital, amesema alikuwa akitoa bure mbegu za uzazi kwa wanawake ambao wanataka kupata watoto wazuri kama yeye.

"Niliamua tu kusitisha sababu nina watoto wa kutosha, sasa hivi kwanza nahitaji kuwalea kwa hiyo hayo mambo mengine baadae, nina mwanamke wangu halafu tunapendana sana yaani kwa kifupi nimehangaika sana naangalia zaidi maisha natengeneza pesa", amesema.




>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

@burudanitele



Distributed via ippmedia

# MASHABIKI WACHOSHWA 'COPY AND PASTE' YA DIAMOND

KUKIRI kwa mtayarishaji wa muziki nchini, S2Kizzy, ambaye ndiye aliyefanya ngoma ya 'Baba Lao' kwamba wimbo unatokana na kazi ya msanii wa Nigeria, Naira Marley, imezidi kuleta hisia tofauti kwa mashabiki.

Akijibu tuhuma hizo amesema kuwa yeye na Diamond walianza kutengeneza wimbo wa 'Baba Lao' muda mrefu sana na hadi kutumia wimbo huo wamepata ruhusa kutoka kwa Naira kupitia wimbo wake 'Soupy'

Hata hivo baadhi ya watu wamepinga dhana hiyo na kuelezea ukubwa wa Diamond hapaswi kuchukua wimbo wa msanii mwingine na kuutengeneza jambo ambalo linaashiria kipaji chake kinaishia ukingoni.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Kama** huna imani na mtu, basi ni rahisi sana kumfikiria na kumdhania vibaya- **Tundaman.**



**Ukichunguza** sana wanawake wengi wanavumilia ndoa lakini si kwamba wanafurahia ndoa- **Shamsa Ford.**



**Kila** binadamu mwenye akili timamu anajua anachokifanya kina maana gani kwenye maisha yake, hata kama kuna mwengine pembeni anaona unachokifanya si sawa,ila ifahamike kuwa wakati mimi unaniona nakosea wewe hujui mimi nakuchukuliaje -**Amber Rutty.**

# Kuumbe!



# AMEJIKAZA KIUME
## JUX AKUBALI YAISHE

SIKU za hivi karibuni mitandao ya kijamii ilitawala gumzo kuhusu mwimbaji wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee kunasa katika penzi zito na kijana kutoka Nigeria, Rotimi.

Vanessa alitangaza uhusiano wake huo mpya baada ya kubwagana na msanii mwenzake Juma Jux, ambaye walidumu kwenye mapenzi kwa muda mrefu.

Hata hivyo, mijadala katika mitandao ilikuwa ni namna gani Jux atalichukulia jambo hilo ikiwa inaeleweka wazi kwamba wawili hao huwa na kawaida ya kuachana mara kwa mara na kurudiana.

Wakati mjadala huo ukipamba moto, Jux amejitokeza wiki hii kuzungumzia suala hilo akisema hajatetereka hata kidogo.

Jibu hilo limeonekana kuongoza moto huo kwenye mkaa kwa mashabiki wao kuhoji inakuaje msanii huyo kusema amefurahi wakati sura yake inaonekana haikuwa na uhalisia?

Katika maenelezo yake Jux amesema amefurahi kumuona mpenzi wake wa zamani, Vanessa Mdee kupata mchumba mpya. Kwani hali hiyo itamrudisha kwenye furaha.

"Kuna muda nilikuwa nasubiri sana kuona Vanessa Mdee aje kuwa tena na furaha, Unajua kwenye mapenzi ikitokea mmoja ameachwa kuna mambo huwa hayaendi sawa, Drama na vitu kama hivyo.. Lakini ikitokea wote mpo kwenye mahusiano mnakuwa sawa na mnakuwa na furaha,"

Aliongeza "Nilichokuwa nahitaji ni amani baina yetu, kwa kweli mimi nafurahi sana naamini kwa sasa anafuraha. By the way nimeangalia tamthiliya ya POWER mara nyingi, Nampenda sana Rotimi jinsi anavyoigiza,", amesema Jux.

Akikazia mazungumzo yake, Jux alikiri kuwa Vanessa ni aina ya mwanamke ambaye kila mwanaume angetaka kuwa nae kwani ni mpambanaji na ni mrembo.

Kutokana na kauli yake hiyo, baadhi ya watu walisema pongezi za Jux kwenda kwa mpenzi wake wa zamani hazina uhalisia na badala yake amejikaza kiume ili aonekane hajaumizwa.

Mmoja wa wachangiaji alikwenda mbali na kusema watu wasiendelee kushupalia jambo hilo kwa sababu wasanii hao wote wanapendana na kwamba kinachofanyika ni kuchezea akili za watu.



# Ngoma zilizonyanyasa mwezi Oktoba



**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Septemba ulikuwa ni kama mwezi wa mafuriko ya wasanii wengi wa Bongo fleva kuipua ngoma zao.

Haijulikani waliingia lini studio, lakini wasanii wengi wametambulisha ngoma zao kuanzia katikati ya mwezi Septemba na kwa kiasI kikubwa zimenyanyasa sana na kuwa gumzo mwezi Oktoba.

Mpaka sasa baadhi zinaendelea kutesa na kuteka mioyo ya mashabiki wa muziki huo nchini.

Hizi baadhi ya ngoma ambazo zimeonekana kutIa fora kwa kutazamwa kwenye mitandao ya kijamii, kupigwa kwenye redio na kwenye vipindi cha televisheni mwezi uliomalizika wa Oktoba.

**Nikagongee remix-Baddest ft Shilole**

Katikati ya mwezi huu, msanii Baddest aliustua ulimwengu wa muziki wa bongo fleva alipotoa ngoma ya 'Nikagongee' ambayo imetia fora.

Ni ngoma iliyopokelewa haraka na kupendwa na mashabiki wengi kiasi cha kuwafanya madj kwenye vipindi mbalimbali kuipiga mara kwa mara.

Kutokana na hilo, akaona isiwe tabu. Akaamua kuitoa tena ngoma hiyo kwa mara nyingine mwishoni mwa Septemba na kuendelea kutesa mwezi Oktoba.

Safari hii akamshirikisha mwanadada Shilole. Kila kitu ni kile kile cha mwanzo. Kuna vionjo vichache tu vimeingizwa na hasa beti ya Shilole. Kwa sasa bado inaendelea kunyanyasa.

**Anyinya-Marioo**

Msanii Marioo mwezi Oktoba naye hakuwa nyuma. Akatoa ngoma yake aliyoiita 'Anyinya'. Ni ngoma ambayo huko mitaani na uswazi imeonekana kupendwa mno na watoto na akinadada, huwezi kupita zaidi ya mitaa mitatu bila kusikia mwanadada au mtoto anauimba. Ni wimbo uliopokelewa vema mno.

**Taa-Marlaw**

Amerejea tena. Mwezi Oktoba umekuwa na 'sapraizi' ya nguvu kwa mashabiki wa ngoma za kizazi kipya kwa ujereo wa mmoja wa wasanii walioiweka na kuifikisha bongo fleva hapa ilipo.

Huyu si mwingine ni Marlaw. Katikati ya miaka ya 2000 alitamba mno na ngoma ya 'Rita' ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo iliyomfanya awe staa. 'Pipii' na nyingine zikaja baadaye.

Sasa amekuja upyaaa na ngoma ya 'Taa' baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu sana.

Ngoma hii imetamba sana mwezi Oktoba na hata mwezi huu inaendelea kutesa kwa sababu wengi wanataka kumuangalia kama kiwango chake kiko vile vile au?

**Bugana-Billnas ft Nandy**

Ngoma hii nayo imesumbua mwezo Oktoba na inaendelea kufanya hivyo mwezi huu wa Novemba.

Wasanii hawa wameungana na kutoa ngoma iitwayo 'Bugana'. Mbali na ngoma kuwa bomba kutokana na jinsi ilivyopigwa, lakini wengi wamekuwa wakiifuatilia kutokana na zile tetesi za wakati ulee wa nyuma kuwa wasanii hawa Billnas na Nandy walishwahi kuwa wapenzi.

**Vua Nguo-Ney wa Mitego**

Nay naye ana mambo. Mwezi Oktoba kaleta kitu ambacho yeye mwenyewe kakiita 'Vua Nguo'.

Si mnamjua tena jamaa jinsi alivyo mtata kwenye ngoma zake? Ngoma hiyo imekuwa ikiwaacha watu hoi na mwezi Oktoba wote ndiyo habari ya mjini. Hata sasa inendelea kubamba kwani ndiyo kwanza ngoma bado mbichi.

# Vijimambo

1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**



# Penzi laumiza Ndoa inayoponzwa na wazazi

**Na Adam Fungamwango**

KUNA baadhi ya wanawake hawana wivu wa maendeleo. Hawana nia ya kuona mpenzi au mumewe anafanikiwa. Yeye yupo pale kwa maslahi binfasi tu.

Na wanawake kama hawa kile kilichomleta pale kikishamalizika, wanaondoka. Hawajali kumuacha mume wala watoto.

Filamu ya 'Penzi Linaumiza' inaakisi hiki ninachokieleza hapa. Imechezwa na wasanii Hemed Suleiman, Kajala Masanja, Fatuma Makongoro, Fatuma Makongoro maarufu kama Bi Mwenda, Hashim Kambi, Hamisa Mobeto na wengineo.

Hemed anatarajia kuoa. Lakini bado hajampata mchumba. Dada yake Kajala ataka amuoe Irene kwa sababu ni shoga yake. Kaka akamkubalia dada yake. Walipokwenda kwa wazazi wa mwanamke wakakutana na mambo ya kushangaza.

Mzee Kambi ambaye ni baba wa binti huyo Irene, akawa anamuuliza anayetaka kuoa mambo ambayo hayahusiani kabisa na ndoa.

Maswali hayo yalipaswa kuulizwa na TRA, au watoza kodi ya majengo au watu wengine wanaohusiana na mambo ya pesa na majengo.

Anamuuliza Hemed kazi anayoifanya, mshahara anaoupata na kama ana nyumba ya kuishi.

Anachojitetea mzee Kambi ni kwamba hataki binti yake aolewe halafu aende kupata tabu.

Ingewa baba haridhishwi na kipato cha mkwewe mtarajiwa, lakini binti alishinikiza mpaka akaolewa.

Kasheshe lilianza ndoa ilipomalizika. Kutokana na maisha ya kudekezwa na wazazi wake, kumbe akawa hajui kupika wala kufua.

Katika kile alichoona kuficha udhaifu na aibu yake kwa jamii, akamshinikiza mumewe wakaishi hotelini. Ikawa hivyo. Siku zote mapenzi ni upofu. Hemed alilazimika kulipia gharama zote za chakula na malazi, ili mradi tu asimuudhi Irene.

Gharama za hoteli ni kubwa, kiasi cha kubaliza pesa zote na kuamua sasa kukwapua pesa za serikali.

Nadhani huyu atakuwa amekwapua pesa za serikali za Awamu ya Tano, maana huwa ni za moto na hazikwapuliki kirahisi kabla ya kushtukiwa.

Wakaguzi wa mahesabu wanathibitisha upoteza wa pesa, Hemed akasimamishwa kazi kwa muda.

Maisha yanaanza kuwa magumu, Irene akarejea kwa wazazi wake, lakini akiwa na mimba wa miezi mitano. Hemed anaamua kwenda kuishi kwa dada yake.

Miezi kadhaa baadaye Hemed anakutaka na shoga ya mkewe njiani na kumtaarifu kuwa amejifungua. Hemed anakusanya nguo za mitumba na vijizawadi kwenda kumpelekea mtoto wake.

Alipofika ukweni alifukuzwa kama mwizi, vinguo akatupiwa usoni na kupigwa mkwara kuwa asifike tena pale.

Hemed anasalimu amri na kuamua kugeukia upande wa pili wa maisha.

Miaka saba baadaye, Hemed akiwa nyumbani kwake, anapokea mgeni, mwanamke akiwa na mtoto mdogo. Walikuwa wachafu na walionekana hawakuwa kwenye maisha mazuri. Ni mkewe Irene na mtoto wake.

Kumbe baada ya miaka kadhaa kupita, iligundulika kuwa baba yake Irene mzee Kambi ni fisadi, hivyo serikali ikataifisha mali zake. Akaamua kurejea kijijini yeye na familia yake yote. Irene alimuoba Hemed Msamaha. Hemed alichofanya ni kumchukua tu mtoto wake, kwani tayari alishaoa mke mwingine ambaye ni Hamisa Mobeto.



# HII KUFURU

## BROWN AUZA NGUO ALIZOTUMIA

USTAA una mambo bwana! Mwanamuziki maarufu Marekani Chriss Brown, amesababisha watu kusubiri kwa muda mrefu kwenye foleni ndefu kwa lengo moja tu, nalo ni kubahatika kununua mavazi ya msanii huyo ambaye alikuwa akiuza kwa mnada.

Mkali hiyo wa R&B nchini Marekani aliendesha mnada nyumbani kwake wa kuuza bidhaa zake ambazo tayari ameshazitumia.

Vitu ambavyo viliuzwa ni pamoja na mapambo ya ndani, nguo na viatu ambavyo alivitumia kwa nyakati tofauti.

Mnada huo wa siku mbili ulianza siku ya Jumatano nyumbani kwake Los Angeles, uliwafanya mamia ya mashabiki zake kujazana wakiwa na nia ya kununua wakiwemo walanguzi.

Hata hivyo watu hao iliwabidi kusubiri kwa muda mrefu kuanza kwa mnada huo na kusababisha malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara ambao walijaribu kupata bidhaa kutoka kwa mwimbaji huyo ili wakawauzie watu wengine au wengine wakavae kabisa.

Brown alituma vipeperushi kwenye akaunti yake ya Instagram na Twitter siku ya Jumanne usiku akiwataka wafuasi wake wenye nia ya kununua vitu hivyo kwenda kwake kuvinunua.

Katika ujumbe huo ulielekeza anwani ya jumba lake lililopo katika kitongoji cha Tarzana kwenye Bonde la San Fernando Los Angeles, huku akiwahimiza watu watakaovutiwa kwenda kupata bidhaa au hata kununua nguo za kuvaa.

Brown, ambaye anajulikana kwa jina lake la utani Breezy, ambalo alililipata jukwaani mnamo mwaka 2005, aliweka mahema kadhaa yaliyosheheni vitu hivyo kwa ajili ya watu kununua.

Mwimbaji huyo alishinda tuzo ya Grammy mwaka 2011 katika kipengele cha albam bora ya R&B, pia albamu yake mpya "Indigo" ilichukua nafasi ya kwanza wakati ilipotolewa Juni, mwaka 2-019, huku wimbo wake wa "No Guidance" featuring Drake ukiwa umechaguliwa kuingia tuzo ya American Music Awards

# Wizkid kuimba Singeli?



MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Wizkid ameonesha nia ya kuingia katika muziki wa Singeli na kutangaza kuimba na msanii Dulla Makabila.

Wizkid ambaye anatamba na kibao 'Joro' ameonekana akifanya mazungumza na msanii wa huyo na video yake kupostiwa katika mtandao wa instagram.

Kufuatia tukio hilo, mashabiki wa muziki huo wamempongeza mkali huyo wa kuimba Singeli kwani hatua hiyo itasaidia muziki huo kuvuka mipaka.



## Ellen kama Card B

MTANGAZAJI maarufu wa Marekani, Ellen ameibua gumzo baada ya watu kumpongeza baada ya kuvaa mavazi rapa Card B katika kusherehekea sikukuu ya 'Halloween'.

Wakiwa pamoja kwenye kipindi cha Televisheni, Card B alivaa nguo za Ellen na mtangazaji huyo alionekana kivutio huku akijiita yeye ni Card E.

Sikukuu hiyo ambayo husherehekewa kila Oktoba 31, watu hufurahia kwa kuvaa nguo mbalimbali za kutisha na kushangaza.


## T.I haya unayosema hawajakuelewa

Distributed via ippmedia

RAPA wa Marekani, T.I. amewashangaza mashabiki wake baada ya kueleza atampeleka binti yake hospitali kuhakikisha kama bado ni bikra.

Kulingana na mtandao wa TMZ, rapa huyo ambaye alikuwa mgeni katika kipindi kimoja cha radio alisema hatua hiyo si kumdhalilisha mtoto wake bali ni kumlindia heshima yake kama msichana.

Kwa mujibu wa T.I. wakati wakiwa hospitali hatoingia katika chumba cha matibabu badala yake atabaki nje na kusubiri majibu kutoka kwa daktari.





## Card B ndani ya Lagos Desemba

RAPA mwenye utata mwingi, Card B hatimaye amethibitisha kwenda nchini Nigeria mwezi Desemba mwaka huu.

Mshindi huyo wa tuzo za Grammy, atawasili jijini Logos baada ya mashabiki wengi kumsubiri kwa muda mrefu tangu atangaze kwenda nchini humo mwaka jana.

Card B atakuwa mmoja wa wasanii wakubwa wa Marekani waliovuka mipaka hadi bara la Afrika kwa ajili ya kufanya kazi za muziki pamoja na utalii.

## Chris Brown huo ni wivu tu

BAADA ya kuweka gulio maalum nyumbani kwake, sasa mwanamuziki Chris Brown amedai polisi walijaribu kumzuia kufanya biashara hiyo.

Chris amesema polisi wa Los Angeles, walimuwekea vikwazo mbalimbali wakati zoezi la kuuza vitu vyake likiendelea ndani ya nyumba yake.

Kwa mujibu wa TMZ, mkali huyo wa R&B amedai kwamba wakati akiendesha mnada huo polisi hao walifika na kumzuia kwa madai walipata simu kutoka kwa jirani akilalamika kwamba kuna watu waliingia katika eneo lake bila ruhusa





## MIONZI YA SHERIA

Na John Juma
0716217615

# Ndivyo unavyodai fidia kutokana na madhara

MADHARA ni matokeo hasi yanayompata mara nyingi mtu au kitu na wakati mwingine mali kutokana na kitendo kilichofanywa na mtu mwingine au kilichotokea kutokana na mtu flani kushindwa kutimiza wajibu.

Kutokana na madhara hayo mtu aliyeumizwa anastahili kupata fidia.

Ili kupata fidia, inampasa mtu aliyepata madhara hayo kufungua shauri la madai katika mahakama yenye mamlaka ili ipime madhara yaliyotokea na kuamuru kulipwa fidia au kutolipwa na ya namna gani.

Ili kufanikiwa katika shauri la kudai fidia kutokana na madhara yaliyosababishwa na

mwingine au mwingine kushindwa kutimiza wajibu wake mambo yafuatayo inabidi yathibitishwe mbele ya mahakama.

Mosi kuwe na wajibu wa kujali au wajibu wa kisheria upande wa mdaiwa fidia.

Wajibu huo uwe umevunjwa na mdaiwa fidia na uvunjwaji wa wajibu huo usiwe umechangiwa na anayedai fidia. Aidha, kuwe na madhara yanayotokana na uvunjwaji wa wajibu upande wa mdai fidia.

Mojawapo ya sheria zinazosimamia madhara inatoka katika Sura ya 310 ya Sheria za Tanzania kama ilivyorejewa mwaka 2002 (The Law Reforms (Fatal Accidents and Miscellaneous Provisions) Act).

Kuna namna mbalimbali ambazo mtu akishindwa kutimiza wajibu wake anaweza kusababisha madhara kwa wengine na kupelekea muathirika kufidiwa. Namna hizo ni kama wajibu wa mwenyeji kuhakikisha kuwa wanaoingia na kutoka kwenye eneo lake kwa halali hawadhuriki.

Mwenyeji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa wote wanaoingia na kutoka katika eneo lake kihalali hawapati madhara.

Akishidwa kutimiza wajibu huo na madhara yakatokea, mtu aliyeumia anaweza kudai fidia. Baadhi ya mifano ya mambo yanayoweza kupelekea madhara kutokea na mtu kudai fidia chini ya wajibu huu ni pale ambapo aliyekwenda kwenye nyumba ya mtu au taasisi na kukuta sakafu inateleza kutokana na kupiga deki au asili ya sakafu bila kuwa na ilani (tahadhari) kuhusiana na hali ya sakafu hiyo na mtu akateleza au akaanguka na kuumia.

Inaweza kutokea endapo mtu amepanda gari la mtu mwingine na gari hilo likawa na viti vibovu na kupelekea abiria huyu kuumia au kupata ajali kutokana ubovu wa gari hilo.

Wajibu wa mtu kulinda hadhi na heshima ya mwingine chini ya wajibu huu, kila mtu ana wajibu wa kulinda hadhi na heshima ya mwenzie.

Distributed via ippmedia

Iwapo atafanya lolote na kusababisha hadhi ya mwenzie kushuka, aliyefanyiwa hayo anaweza kudai fidia. Mfano wa uvunjifu wa wajibu huu ni pale A amefanya tendo au amesema maneno ambayo si maoni halali juu ya mtu B mbele ya watu wengine na kwa maoni ya hao watu wengine tendo lile au maneno yale yanashusha hadhi au yanamdhalilisha mtu B. Kisheria B anaweza kwenda kudai fidia.

Halikadhalika wajibu wa mtu kutoharibu raha na furaha ya mwingine, wajibu huu unamaanisha kwamba mtu hatakiwi kuwasumbua wengine walioko jirani naye.

Mfano wa uvunjifu wa wajibu huu ni pale ambapo mtu anasababisha karaha kwa kufungua mziki kwa sauti ya juu bila kibali au bila kuzingatia masharti ya kibali.

Jingine ni kusababisha harufu

mbaya kiasi cha kuwakosesha raha au kuwasumbua wengine. Wajibu mwingine ni wa mwenye mali au mwajiri kuhakikisha kuwa mawakala au wafanyakazi wanatimiza wajibu wao kwenye kazi au ajira haiwasababishii madhara kwao na kwa wengine.

Wajibu huu unamaanisha kwamba, mwajiri au mwenye mali ana wajibu wa kuhakikisha kuwa

mawakala au waajiriwa wake hawasababishi madhara kwa wengine wakati wanatimiza majukumu yao ya kazi.

Mfano wa uvujifu wa wajibu huu ni pale ambapo mfanyakazi au mwajiriwa binafsi au kwenye taasisi au wakala akifanya kitu chenye kuleta

madhara kwa mtu mwingie au juu ya mali ya mwingine wakati anatimiza majukumu yake. Hili likitokea aliyepata madhara, au mali yake anaweza kudai fidia kutoka kwa mwajiri au mwenye mali. Mfano, mwingine ni pale ambapo mtu amepanda basi gari na akapata ajali au kuumia akiwa kwenye basi hilo na kapata madhara anaweza kudai fidia kutoka kwa dereva aliyekuwa akiendesha gari hilo pamoja na mmiliki wa gari au basi hilo.

Mara nyingi hii ni pale ambapo basi au gari lilikuwa ni la biashara mfano mabasi yanayosafirisha abiria.

Wajibu wa watawala na viongozi kuhakikisha hawafanyi vitendo ambavyo vitawaathiri wananchi wao.

Chini ya wajibu huu, viongozi au watawala wanapaswa kujali na kufanya mambo ambayo hayaleti madhara kwa wananchi wanaowaongoza.

Mfano kiongozi anaruhusu takataka zitupwe kwenye eneo fulani ambalo lipo kwenye makazi watu.

Cha kuzingatia ni kila mtu ana wajibu wa kujali na kuhakikisha kuwa kitendo chochote anachofanya hakisababishi madhara hasi kwa mwenzake.



## KALAMU YA MWALIMU

Na Reubeni Lumbagala

# Walimu tuna fursa nje ya ufundishaji

NI jambo muhimu linalotamaniwa na kila mtu kufanya shughuli zaidi ya moja kwa ajili ya kujiongezea mapato. Ni kutokana na ukweli kuwa hakuna chanzo kimoja cha kipato kinachoweza kutosheleza mahitaji yote ya binadamu. Ndiyo maana wanauchumi wanashauri mtu kuwa na vyanzo ya kujiingizia kipato zaidi ya kimoja ili kuweza kutimiza mahitaji ya msingi na kufanya maendeleo mengine muhimu kwa ajili ya ustawi wa maisha.

Walimu kama watu wengine kwenye jamii, nao wanapaswa kuwa na shughuli za ziada za kujiongezea kipato nje na kazi yao ya ufundishaji ili kuweza kumudu kuendesha maisha yao kwa mafanikio.

Na ndiyo maana baadhi ya walimu wanajishughulisha na kilimo, ufugaji, biashara, kuandika vitabu na kufundisha masomo ya ziada (tuition) ili kuweza kupata kipato cha ziada.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina utaratibu wa kusimamia na kuratibu Mashindano ya Michezo na Sanaa kwa Vyuo vya Ualimu Tanzania Bara (Umisavuta) ili kuweza kuibua na kuendeleza vipaji vya walimu kupitia mashindano hayo.

Ufunguzi wa mshindano haya kwa mwaka huu, umefanyika mwezi uliopita (Oktoba 27, 2019) katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Katika ufunguzi huo Waziri wa Habari Dk. Harrison Mwakyembe, alikuwa mgeni rasmi, akimwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Mashindano hayo yaliyofanyika kwa takribani wiki moja yalishuhudia washiriki zaidi ya 5,600 kutoka katika vyuo vya umma vya ualimu 35.

Mashindano ya Umisavuta yamejumuisha michezo ya aina mbalimbali kama vile mpira wa miguu, wavu, kikapu, pete na riadha. Kwa upande wa sanaa, imejumuisha ngoma, uchoraji, kwaya, maonyesho mbalimbali. Baada ya ufunguzi wa mashindano hayo, viwanja vya michezo vya vyuo vya Ufundi cha Ualimu Mtwara vilitumika kuendesha michezo na sanaa hizo kwa walimu washiriki.

Pamoja na walimu kusomea taaluma ya ualimu ambayo wanawajibika moja kwa moja katika kuwafundisha wanafunzi na kuwapatia maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali lakini wanayo fursa ya kutumika vipaji vyao walivyojaliwa na Mungu katika kujiongezea kipato nje na mishahara yao ya ualimu.

Mashindano hayo si tu kwa ajili ya kujenga afya na burudani lakini pia ni njia mojawapo ambayo walimu wakiitumia vyema inasaidia katika kuwapatia walimu fursa za kiuchumi. Mashindano haya huwashirikisha wadau mbalimbali ambao kwa njia moja au nyingine wanatafuta wanamichezo na wasanii wa sanaa mbalimbali.

Hivyo basi, Umisavuta ni njia ya kujinadai na kujitangaza kwa wadau wanaotafuta vipaji mbalimbali. Mathalani, walimu wenye vipaji katika michezo ya mpira wa miguu, pete, kikapu wavu au riadha wanaweza kuchukuliwa na kujiunga na timu mbalimbali.

Fursa hii inawapa walimu wasaa wa kuendelea na kazi yao ya ufundishaji huku wakitumia muda wa ziada katika michezo hiyo.

Aidha, walimu wenye vipaji vya uchezaji na upigaji wa ngoma za asili, uimbaji, uigizaji na uchoraji, wanaweza kujipatia kipato cha ziada kupitia sanaa hizi.

Halikadhalika walimu wanaweza kutafuta fursa katika magazeti na majarida mbalimbali katika uchoraji wa picha na katuni ili kutoa elimu kupitia uchoraji.

Vipo vikundi vya uimbaji na wachezaji wa ngoma ambavyo vinatumbuiza katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiserikali, walimu wenye vipaji vya uimbaji, kucheza au kupiga ngoma wanaweza kupata fursa hii adhimu na kutunisha mifuko yao.

Kwa hiyo, walimu wawapo vyuoni wakijifunza taaluma ya ualimu, watambue kuwa wanaweza kutumia vipaji vyao katika kuongeza thamani ya maisha yao kwa kupata kipato ziada nje na ufundishaji shuleni au vyuoni.

Mashindano haya yawe chachu na yawaamshe walimu katika kutumia vipaji na karama walizonazo kujitangaza kibiashara badala ya vipaji vyao kutumika kama burudani pekee.

Wanamichezo na wasanii ni watu wenye vipato vikubwa duniani na kupitia michezo na sanaa wanazozifanya, wamejikuta wakiwa mabilionea na mamilionea. Kwa mantiki hii, walimu nao wanaweza kuwa mabilionea na mamilionea kama watatumia vipaji vyao ya michezo na sanaa badala ya kubaki na kazi moja ya ufundishaji huku wakiwa wamebarikiwa kwa kuwa na vipaji lukuki vinavyohitajika katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na nje ya nchi.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ihakikishe Umisavuta inakuwa endelevu ili kuendelea kuwatengenezea fursa walimu na kukuza umoja baina ya vyuo vya ualimu.

Pia serikali ivishirikishe vyuo binafsi vya ualimu ili nao waweze kushiriki na kuibua vipaji vya walimu. Walimu nao wasibaki nyuma katika kushiriki kikamilifu katika mashindano haya na kuchagua michezo na sanaa ambazo wanaweza kufanya vyema kitaifa na kimataifa. Tutafakarini walimu.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

# MAAJABU

## • Kutoka 'wadunga mimba' wana mitandao kufuatilia

**Na Gaudensia Mngumi, MAFIA**

KUNA msemo kuwa mchawi mpe mwana alee. Hilo ndilo linalofanyika kisiwani Mafia katika Mkoa wa Pwani kwa sasa. Analea mwana kwa sababu watuhumiwa namba moja wa kuwapa wanafunzi mimba ambao ni madereva wa bodaboda, wamebadilika na ndiyo walinzi na watetezi wa mabinti iwe shuleni au mitaani.

'Wachawi' hawa ni walinzi wa wasichana na mabalozi wa wakupinga vita mimba za utotoni, ukatili kijinsia na kuwanyanyasa watoto kingono.

Hivi karibuni Nipashe ilifika Mafia na kukutana na mwamko mpya wa bodaboda ambao ni chachu na chanzo cha mabadiliko na walinzi na watetezi wa watoto na wapinzani wakubwa wa ndoa za udogoni kisiwani humo.

Kwa mujibu wa Selemani Haji, Mtendaji wa Kijiji cha Muburani moja kati ya vijiji 23 vya Mafia, ambacho kina sekondari ya Micheni (shule ya kata), kila mara wanafunzi wa shule hiyo walipopata mimba waliwataja madereva wa pikipiki.

"Kila kesi inayofikishwa ofisi ya kijiji, mwanafunzi anamtaja bodaboda. Walihusika kwa vile wana pesa za papo kwa papo, usafiri wa haraka wa kumfikisha binti shule na kumpeleka sehemu yoyote." Anasema Haji.

Anaeleza kuwa madereva hawa walionekana na wanafunzi wakiwa hata nyumbani kwao na pia kwenye pikipiki zao na kwa ujumla walikuwa watuhumiwa wakuu kila kesi ilipoibuliwa.

Anaeleza kuwa mabinti walikuwa wahanga kwani wengi hawana usafiri wanatembea zaidi ya kilometa tano kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Aidha, msaada wa karibu kwao ni bodaboda ambazo kwa wanafunzi wengi hawana fedha za kulipia usafiri wala baiskeli, hivyo hutegemea huruma ya lifti ya pikipiki, mwisho wa msaada huo ni hadaa za mapenzi zinazoishia na mabinti kupata mimba.

**MBINU ZILIZOTUMIWA**

Katika ziara ya wanahabari wilayani Mafia iliyoandawaliwa na Shirika la Action Aid Tanzania (AATZ), kutembelea miradi na wanajamii wanaohudumiwa na shirika hilo, Nipashe ilifika katika Shule za Msingi Balemi na Kilindoni na katika kuzungumzia hadaa na ubakaji unaofanywa kwa wanafunzi, wanataja madereva wa pikipiki na mbinu wanazotumia.

Wanataja mbinu kama madereva kuwapa lifi wanafunzi, kuwanunulia mabinti simu, kuwawekea fedha za matumizi kwenye simu na pia kuwatumia 'mshiko' na kuwarubuni kupitia mawasiliano hayo.

Wanadaiwa kuhusika na kuwapeleka mabinti kwenye nyumbani zao, wengine walitumika kuwafikisha kwenye nyumba za wageni au mafichoni ambako wananyanyaswa kingono aidha, wanawapeleka wavulana maporini na kuwalawiti.

Vilevile, wanafunzi hawa wanaeleza kuwa mbinu nyingine zinazotumiwa na madereva hao ni kuwapa watoto wa kiume fedha pengine Sh.10,000 kwa ajili ya kusaidia kuwapata dada zao au kuchonga mchongo wa kuwaletea wasichana wanaowataka.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kilindoni, Stephen Mlobi, anataja njia nyingine iliyotumiwa na madereva hao na watu wengine wanaowawiti watoto kuwa ni kuwaonyesha picha za ngono kwenye 'simu janja' (smartphones) na kuwashawishi kufanya ngono kinyume cha maumbile.

Anasema kwa kutumia simu na hata televisheni nyumbani, kuwapa fedha na zawadi watoto hawa wa kiume wanakubali kuonyeshwa picha hizo na kutumbukia kwenye unyanyasaji huo.

**MWANZO MABADILIKO**

Mratibu wa Action Aid, Wilaya ya Mafia, Samwel Mesiaki, anaelezea jinsi AATZ ilivyoleta hamasa kuwabadilisha bodaboda kutoka kwenye kutuhumiwa kunyanyasa watoto na kuwaingiza kwenye ubalozi, ulinzi wa wasichana na machampioni wa kupinga ukatili wa kijinsia na kingono dhidi ya watoto.

Anasema pengine ni AATZ Mafia ndiyo wa kwanza kuwatumia madereva hawa kuwa chachu ya mabadiliko. Na kwamba ili kupanga mikakati ya kukabiliana na unyanyasaji wa watoto kingono, waliwaunganisha na kuwahamasisha madereva hawa kuwa mabalozi jambo ambalo limefanikiwa.

Mesiaki anaielezea Mafia kuwa kuna ukatili wa kijinisia na kingono dhidi ya watoto na pia suala la muhali au jamii kuoneana aibu au haya na kumwona mtuhumiwa wa ukatili huo kuwa ni jamaa na ndugu wa karibu asiyeweza kuchukuliwa hatua, ni suala linalorudisha nyuma kukomesha vitendo hivyo.

Hata hivyo, anaeleza kuwa madereva hawa wameleta mabadiliko. Idadi ya mimba utotoni zimepungua, wasichana wanaomaliza darasa la saba ni wengi zaidi na utoro unapungua na unaelekea kwisha ni moja ya mafanikio, AAT inayojivunia.

Mabalozi 155 wamesajili na wanafanyakazi na AATZ Mafia, lakini jitihada zinafanyika kuongeza idadi ili kuwa na walinzi wengi na watetezi wa watoto, anaongeza Mesiaki.

**MTANDAO WA ULINZI**

Kuunda mtandao huo ni moja ya mikakati. Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Pikipiki Mafia (Chawapima) Omary Khai, anapozungumzia juhudi hizo anasema kuna wanachama takriban 730 kisiwani kote ambao ni mabalozi wa kupinga unyanyasaji watoto.

Aidha, ili kukomesha ukatili huo wameunda vikundi au vijiwe 42 vipo kila mahali Mafia na wamekubaliana kuwalinda, lakini pia kuwafichua wote wanaowanyanyasa watoto kingono, anasema Khai.

"Tunafuatiliana kwenye vijiwe tukikukamata tunatoa ripoti polisi. Tunao mtandao ambao tunadhibiti uhalifu kuanzia kunyanyasa watoto, biashara haramu za dawa za kulevya na bangi,"anasema Khai.

Mwanachama wa Chawapima, Daniel Peter, anaelezea zaidi namna ya kutimiza wajibu huo kwa kuwalinda watoto kupitia mtandao maalumu uliounganishwa na jeshi la polisi ambao kila wanapoona kuna dalili za udhalilishaji binti au watoto wanafuatilia kuwaarifu polisi.

"Tumekubali kuwalinda watoto wetu. Tunajua asipokuwa mwanao ni wa ndugu yako. Ni raia wa taifa hili. Sisi ni mabalozi tuliojitambua."

Aidha, Peter anasema pikipiki ndiyo usafiri mkubwa Mafia na kwingineko nchini, ndizo zinazotoa huduma kwa asilimia 95 na kwamba wao ni kila kitu kwenye kusafirisha.

Ni kwasababu wapo kila kona, wametapakaa nchi nzima, wanapenya pale magari yasipofika na ni miongoni mwa wachache wenye kipato ndani ya jamii, hivyo ndiyo wahusika wakuu wa ulinzi wa mtoto.

"Baada ya kuhamasishwa na



Wanafunzi wa Shule za Msingi Kilindoni na Balemi, wakicheza ngoma kuhamasisha mabadiliko ya tabia na kuacha ukandamizaji wa watoto wa kike.

**MAKALA**

# BODABODA

## sasa walinzi wa mabinti,
## a, kuripoti unyanyasaji



Mratibu wa Action Aid Mafia, Samuel Mesiaki (kulia), pamoja na baadhi ya madereva wa daladala wa mjini Mafia, wakati wa kujadili mikakati ya kuendeleza jukumu la kulinda watoto wa kike na kupinga ukatili dhidi ya wasichana.

AATZ sasa tunalinda watoto, kupunguza unyanyasaji, mimba za udogoni na tumekubali kwa hiari yetu.

"Tunaona tuwajibike kwa kuwa wasichana kupewa mimba ni kuongeza umaskini kwa vizazi vya sasa ni vijavyo. Binti atakosa elimu na kiuchumi hataweza kujikimu. Atazidi kuwa maskini atapata watoto wake na uzao wake wataendelea kuwa maskini."anasema dereva Ali Bakari.

Anasema hilo tunalifanya lakini pia tunakuwa mabalozi wa kuieleza na kuikumbusha jamii yetu kuwa ni lazima tujitambue na kuachana na mazoea hayo yasiyokuwa na tija.

Dereva Maulidi Mpogo, anasema bodaboda ni wepesi na popote pale wanafika ni jukumu la taifa sasa kuwahamasisha na kuwatumia kukomesha uhalifu wa aina mbalimbali ukiwamo ukatili dhidi ya watoto.

### WANATOA USHAURI

Kwa serikali, Mwenyekiti wa Chawapima, Omary Khai, anashauri iwashirikishe madereva hao kikamilifu kwenye masuala ya usalama, ulinzi wa watoto na taifa pia.

Anaiomba iwawezesha kufika mikoa mbalimbali kufikisha ujumbe wa kutumiwa kuleta mabadiliko na kusaidiwa kuwa na chombo cha umoja wa wasafirishaji hao ambao ni muhimu nchini.

Kwa madereva wa boda wanakumbushwa kuwa waadilifu na kufuata sheria lakini pia kuwa na hofu ya Mungu kwa kusali na kushiriki ibada.

Aidha, madereva hao wanashauriwa kutumia ujumbe wa kuhamasisha mabadiliko mfano baadhi ya maneno wanayoyaandika kwenye pikipiki yawe na ujumbe kuwa sisi ni walinzi wa watoto , au ni wanabadiliko tunaopinga ndoa na mimba za utotoni au tuwalinde watoto na kuwasaidia kutimiza ndoto na kujenga maisha yao.

### KUKABILI CHANGAMOTO

Kutokana na kuwa na mwenendo mbaya madereva hawa wa Mafia wanakiri kuwa jamii inawaona wengine kote nchini kuwa ni kundi la wahuni na wahalifu, wezi na wanaowahadaa na kuwarubuni watoto wa kike. " Bodaboda tuna sifa mbaya wakati mwingine wazazi wanakataa posa tukitaka kuoa watoto wao. Wanatuita wahuni. Yote haya yamesababisha kupuuzwa na kudharauliwa kutokana na kukosa uadilifu. Lakini sasa tumejitambua kuwa tuna nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko nchini." Madereva hawa wanasema walifanyakazi bila kujitambua walijitumbukiza kwenye usafirishaji bila kuwa na elimu ya kujithamini na kujipanga kutumikia taifa ndiyo maana wakaonekana kuwa wasio na maadili.

Hata sasa katika sehemu nyingi sifa si nzuri, hawafanyikazi kwa kujiamini kutokana na kutokujitambua huku jamii ikiwachukulia kuwa ni wahuni, anabainisha Daniel Peter.

### TAMKO LAO


Katika mkutano na wanahabari, maofisa wa AATZ na wanajamii kujadiliana mafanikio ya kulinda na kuwa mabalozi wa kuwatetea watoto wa kike, bodaboda wanatoa tamko la kuunga mkono hukumu ya Mahakama ya Rufani ya kukataza ndoa kwenye umri mdogo. Kwa niaba ya wote Mwenyekiti wa Chawapima, Khai anazungumza:"Tunapenda kuwaambia wenzetu kubeba watoto kwa nia ya kuwashawishi na kuwarubuni kingono watoto wa chini ya miaka 18 na wanafunzi tulichukulie jambo hilo kuwa ni hatia. Tena ni jinai kwani ni kuwapoteza watoto ambao ndilo taifa la kesho. Lakini pia ni kukwamisha ndoto na maendeleo yao."

Anataka waendesha pikipiki kuwa na hofu ya Mungu na kwenda kwenye ibada za madhehebu yao kama njia ya kuleta mabadiliko ya kiroho. Anawahimiza wazazi kuzingatia jukumu la kuwalea watoto kimaadili na kujali hatma zao muda wote kwani wengi wamejisahau ndiyo maana watoto wanatumbukia kwenye ngono, mimba za udogoni na uhalifu.

Ali Bakari anawaasa madereva popote walipo kuwaogopa watoto wa chini ya miaka 18 na wanafunzi kama nyara za serikali.

Aidha, anawakumbusha wanaume kujifunza na kuijua adhabu inayotolewa na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya kifungo cha miaka 30 jela kwa anayebaka mtoto wa chini ya miaka 18 au mwanafunzi wa na pia kifungo cha maisha kwa wanaowanajisi watoto wadogo kwani adhabu zipo na wengi wanaweza kuishia jela.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 19 00)



Dondoo: Kulia

1. Kisiwa Unguja na Pemba
6. Mke wa Abrahamu
7. Nyumba ya vitu vya kale
11. Mwanzo 12. Boma
14. adhimu, tukufu
15. Saratani
16. begi 18. Nguo ya Syria
21.Chukua madaraka kwa muda
22.Mtu asiye na maamuzi
24.Kitu cha kufungia
25.Kamba ya viatu
26. Ngoma ya wazaramo
28. Muziki wa mwambao
29. Ficha
30. Adhibu

Dondoo: Chini

1. Kale 2. Chukua maneno ya mtu
3. Piga ramli 4. Goli
5. Shule wa watoto wadogo
6. Aina mojawapo ya Waislamu
8. Wazee 9. Mume
10.Katibu mkuu CHADEMA aliyejiuzuru 13.Mbuga Tanga
16. Mambo muhimu yanayoelezwa
17. Hutumika kukatia vitu
18. Kifungu cha maneno yaliyokamilika 19. Mfereji
20.Mzizi unaoliwa Peru
22. Nabii 23.Hutumika kuvua samaki 25. Ala ya muziki

### Jibu Na: 18

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | N | Y | A | P | A | R | A | | M | | | K |
| N | | E | | | | A | | B | A | N | D | A |
| Y | A | M | K | I | N | I | | | D | | | R |
| W | | E | | N | | | | T | A | N | I | A |
| A | I | N | I | S | H | W | A | | H | | | N |
| N | | I | S | H | A | | | K | A | M | B | I |
| Y | | | H | A | R | U | S | I | | | A | |
| W | A | L | I | | A | S | H | A | N | T | I | |
| A | | | R | | K | I | A | M | U | | N | |
| | A | M | I | N | I | | N | A | N | G | A | |
| | S | | N | | S | | G | | U | | | D |
| K | I | T | I | | H | | A | Z | A | N | I | A |
| | A | | | K | A | D | A | | | | | I |

# CHINA Vs USHIRIKA

# Kujenga viwanda na Runali, vitachakata mbaazi, ufuta

Na Sabato Kasika

SEPTEMBA mwaka huu Shirikisho la Vyama vya Ushirika la China (ACF-SMC), lilivialika vyama vya ushirika kutoka Tanzania, Zimbabwe, Msumbuji, Congo na Kenya.

Lengo la mwaliko huo lilikuwa ni kujadili shughuli mbalimbali za ushirika na jinsi ya kusaidia kuhakikisha njia hiyo muhimu ya kufikia maendeleo inaimarika ili kukuza uchumi kwa wanachama na nchi zao.

Kwa upande wa Tanzania, Chama Kikuu cha Ushirika kinachoundwa na wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale mkoani Lindi (Runali) kilipata mwaliko huo na kuwakilishwa na mwenyekiti wake Hassan Mpako.

Muda mfupi baada ya kurejea Mpako anazungumza na Nipashe kueleza kile kilichojiri kwenye mkutano huo akitaja baadhi ya mambo kuwa ni pamoja na uwekezaji wa pamoja kwenye kuongezea mazao thamani.



Mwenyekiti wa Runali, Hassan Mpako (kulia), akizungumza kwenye moja ya mikutano ya chama hicho.

**KUJENGA VIWANDA**

Pamoja na mikakati mbalimbali waliyojadili, Mpako anaiambia Nipashe kuwa Runali iliiomba shirikisho liangalie uwezekano wa kujenga kiwanda cha kuongezea thamani mbaazi na ufuta ili kuziongezea thamani kabla ya kusafirishwa kwenda kuuzwa nje ya nchi.

Anasema, katika ziara hiyo alifanya mazungumzo na uongozi wa ACFSMC na kujikita zaidi kwenye nyanja za masoko na viwanda, hatimaye wakafikia makubaliano hayo ya ujumbe wa shirikisho hilo kwenda mkoani Lindi.

**ACFSMC KUJA NCHINI**

"Katika mazungumzo yetu tulikubaliana kuwa ujumbe wa ACF-SMC utakuja nchini mwezi huu kufuatilia makubaliano hayo ili hatimaye mtambo huo uletwe kwa ajili ya kuchakata mazao hayo," anasema Mpako.

Kwa mujibu wa Mpako shirikisho hilo lilikubali kuangalia ushirikiano kati ya uwekezaji wake na Runali kwenye uchakataji wa mazao hayo ili kuyapatia masoko ya uhakika duniani.

Anasema shirikisho hilo liliahidi kuagalia kile ambacho Runali inakifanya, ili hatimaye wafikie makubaliano ya kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao yanayokusanywa na chama hicho kabla hayajauzwa.

"Wenzetu China wako juu sana kimaendeleo katika masuala ya viwanda na masoko. Tulizungumza nao na kuwaeleza mahitaji yetu, hasa kwenye masoko ili kuondokana na kuuza malighafi," anasema.

**MATARAJIO YA CHAMA**

Mwenyekiti wa Runali anasema, uimara wa shirikisho hilo utasaidia kuimarisha Runali, ambayo katika bajeti yake ina mpango wa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya wanachama wake kabla ya kuyapeleka katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Runali tuna mpango wa kujenga kiwanda cha kubangua korosho kule Liwale na kingine cha kuchakata mbaazi, hivyo tunaamini malengo yetu yanaweza kutimia iwapo ujumbe huo shirikisho hilo utakapokuja nchini," anasema.

Anasema, hadi nusu ya mwaka huu wa 2019, mauzo ya shirikisho hilo yamefikia dola 319.6, yakiwa yamepanda kwa asilimia 6.6 na kutengeneza faida ya asilimia 3.1 katika viwanda vya bidhaa za kilimo.

Mpako anasema, shirikisho hilo linawakilisha vyama vya ushirika vya China, ambavyo ni chachu kubwa ya mabadiliko ya uchumi kwa familia hasa zinazoishi vijijini, hivyo hata Runali inataka kupata uzoefu huo.

Anasema, shirikisho hilo lina mchango mkubwa katika kuhakikisha kilimo kinafanyika kwa tija, ujenzi wa viwanda vya mazao yatokanayo na kilimo na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwamba kwa uzoefu wake, Runali inaweza kufanikiwa kuwa na viwanda vya kuchakata mazao hayo na kupata mapato kutoka kwa wanachama wake na kuwa katika nafasi ya kuisaidia serikali kuwa na viwanda.

ACFSMC wanataka kuhakikisha Runali inakuwa na uwezo wa kusafirisha korosho kwenda kwenye masoko ya kimataifa zikiwa zimechakatwa, hivyo anaamini hayo yakifanyika, chama hicho kitaimarika zaidi.

**HISTORIA NA MALENGO**

Akizungumzia historia Mpako anasema, chama hicho kilianzishwa mwaka 2013 kikiwa na wanachama 52 baada ya kujiengua kutoka katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Lindi (Ilulu).

"Wanachama wanaounda Runali ni vyama vya ushirika vya msingi kutoka wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, na hadi sasa wapo zaidi ya 100 na wanaendelea kuongezeka," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, tangu chama hicho kianzishwe kimepata mafanikio, ikiwamo kuanzisha miradi ikiwamo ujenzi wa ofisi ya chama iliopo mjini Nachingwea, ghala la kuhifadhia magunia na pemebejeo.

"Runali pia inaendelea kujenga vituo vya maandalizi ya malipo ya wakulima wilayani Nachingwea, ambavyo vitagharimu Sh. milioni 280, huku ujenzi wa ghala kuu mjini Ruangwa nao ukiendelea," anasema.

Aidha, anataja mikakati zaidi ya chama hicho kuwa ni kununua eneo la eka 500 kwa ajili ya shambadarasa la mikorosho ili wanachama wa Runali waweze kujifunza kilimo bora cha korosho, hatimaye wanufaike nacho.

Mpako anaongeza kusema kuwa, chama hicho kina mpango wa kuhamasisha kilimo cha alizeti, ili kiwe na umaarufu mkoani Lindi kama ilivyo kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini.

"Unajua huku kwetu, wakulima wanategemea korosho, ufuta na mbaazi kama mazao makuu ya biashara, lakini sasa tunaongeza alizeti, kwani ni zao ambalo halitegemei soko la nje," anasema.

Akizungumzia mkakati wa kuhamasisha kilimo cha alizeti, Mpako anasema, Runali ikiwa na mapato ya ziada, itanunua mbegu za zao hilo na kuzigawa katika shule za msingi, sekondari na kwenye ofisi za serikali za vijiji.

Mbegu hizo zitagawiwa, ili kuanzisha mashamba darasa, ambayo yatasaidia wakulima wetu kujua namna ya kulima zao hilo na kupata mavuno mengi na kuifanya Lindi kuwa juu kwa kilimo cha alizeti," anasema.

## HABARI KIMATAIFA

# UN yataka mkataba wa amani S/Kusini JUBA, Sudan Kusini

ZIKIWA zimesalia siku 3, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN), limezitaka pande zinazozozana Sudan Kusini, zitangaze hadharani wajibu wao wa kutekeleza makubaliano ya amani yanayotaka iundwe serikali ya mpito ya umoja wa kitaifa Novemba 12.

Taasisi hiyo muhimu zaidi ya ulinzi wa usalama na amani duniani, ilitoa taarifa inayoelezea wasiwasi wake, baada ya wajumbe wake kufika ziarani hivi karibuni nchini humo na kushindwa kuona maendeleo yoyote makubwa katika kutekeleza vifungu muhimu vya makubaliano hayo ya amani yaliyosainiwa mwaka mmoja uliopita.

Kwa mujibu wa mkataba huo, kiongozi wa upinzani Riek Machar, anapaswa kurejea katika mji mkuu Juba Novemba 12, na kukabidhiwa kwa mara nyingine tena wadhifa wa Makamu wa Rais na Dk. Salva Kiir, hiyo ikiwa sehemu ya kugawana madaraka ili kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vimedumu kwa miaka mitano na ambavyo vimesababisha vifo vya takriban watu 400,000, na mamilioni wakiachwa bila makazi na mali.

Mnamo Oktoba 20, Machar alikutana na wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mjini Juba na akaonya kuwa makubaliano ya amani yaliyofikiwa mwaka uliopita yanaweza kuvunjika ikiwa serikali ya umoja wa kitaifa itaundwa kama ilivyokubaliwa Novemba 12.

Badala yake alitaka muda wa kuunda serikali hiyo urefushwe.

Oktoba mwaka jana taarifa kutoka Juba zilieleza kuwa serikali ya umoja wa kitaifa Sudan Kusini ilikuwa kwenye hati hati.

Wakati huo upinzani nchini Sudan Kusini ukiongozwa na Machar uliishutumu serikali kwa kushindwa kufanikisha mkataba wa amani na kutoa wito wa kuchelewesha kuundwa serikali ya umoja wa kitaifa kwa kipindi cha miezi sita.

***DW***




Rais Donald Trump

# Mbabe Agathon Rwasa anadai kutishiwa kifo

**BUJUMBURA, Burundi**

KIONGOZI wa chama kikuu cha upinzani nchini Burundi, Agathon Rwasa, amelaani mpango aliodai unaandaliwa wa kutaka kumuua.

Ikiwa ni miezi takribani mitano imesalia kabla ya nchi ya Burundi kufanya uchaguzi mkuu, kiongozi wa chama kikuu cha upinzani nchini humo cha CNL, amelalamikia kuhusu kile alichosema ni njama za serikali kutaka kukifuta chama chake.

Mbabe huyo wa zamani wa kivita alisema anazo taarifa kuwa idara za usalama nchini Burundi zinapanga kumzushia uasi kama njia ya kumuua au kumtia mbaroni, madai yake anayotoa wakati huu wafuasi wa chama hicho wakiripotiwa kushambuliwa, kuuawa na hata ofisi zao kuchomwa moto na watu wasiofahamika.

Taarifa hiyo iliyothibitshwa na katibu mkuu wa chama cha CNL, Simon Bizimungu, ilisema :"Tunazo taarifa za kweli zinazosema kuwa kuna mpango unaondaliwa katika ngazi ya kitaifa kuhusu kuuawa kwa viongozi wa chama cha CNL na kuwazuia jela baadhi yao. Mpango unawalenga viongozi wa juu wa chama, ikiwa ni pamoja na Agathon Rwansa. Mpango huo unaadaliwa na chama tawala CNDD-FDD na viongozi mbalimbali katika jeshi na polisi", alisema Simon Bizimungu. "Mpango huo unalenga kuwapa watu silaha na sare za chama cha CNL, ili waonekane kuwa ni wapiganaji wa chama cha CNL na mwendesha mashitaka atachukuwa hatua papo kwa papo za kuwakamata viongozi mbalimbali wa chama na kukifuta chama cha CNL, huo ndio mpango unaoandaliwa sasa, " aliongeza Agathon Rwasa.

Hata hivyo Rwasa, alieleza zaidi kuwa hana nia yoyote ya kuingia msituni au kutoroka nchi yake.

Kufuatia visa vya mauaji na mivutano ya kisiasa inayoendelea nchini Burundi, ikiwa imesalia miezi isiozidi saba kabla ya kufanyika uchaguzi wa urais nchini humo, hali ya kisiasa nchini humo inatisha na kuuweka mustakabali wan chi hiyo shakani.

Visa vya kuteketeza kwa moto ofisi ndogo za chama kikuu cha upinzani cha CNL, katika maeneo mbalimbali ya nchi humo vinaendelea, huku chama hicho kikinyooshea kidole cha lawama vijana kutoka chama tawala, CNDD-FDD, Imbonerakure kuhusika na visa hivyo.

Hata hivyo vuguvugu la vijana hao, ambao Umoja wa Mataifa unalitaja kama kundi la wanamgambo, limefutilia mbali madai hayo na kusema kwamba chama cha CNL kinachoongozwa na mbabe wa zamani wa kivita Agathon Rwasa, kinaendelea kupaka matope vijana wake kwa madai yasiyoeleweka.

***Redio Ufaransa.***

# Trump atakiwa kulipa dola milioni mbili

**NEW YORK, Marekani**

JAJI wa Jimbo la New York, Saliann Scarpulla, ameamuru Rais Donald Trump, kuzirudisha dola 2,000,000 alizozichukua kwa matumizi yanayotajwa na mahakama kuwa ni kinyume cha sheria.

Fedha hizo ni kutoka mfuko wa misaada wa 'Trump Foundation', ambapo inadaiwa kwamba alizichukua na kuzitumia katika kampeni zake kwenye uchaguzi wa mwaka 2016 uliomuingiza madarakani.

Uamuzi huu ni sehemu ya mashitaka yaliyowasilishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Jimbo la New York dhidi ya mfuko wa misaada wa 'Donald J Trump Foundation' akiwemo rais mwenyewe na watoto wake watatu Donald Junior, Ivanka na Eric.

Mahakama pia ilielekeza watoto wa Rais Trump wanaosimamia uendeshaji wa mfuko huo kupatiwa mafunzo ya uongozi na kujua namna ya kufanya maamuzi ya matumizi ya fedha kwa misingi inayokubalika kisheria.

"Donald Trump Jr, Eric Trump na Ivanka Trump - ambao pia walikuwa wakurugenzi wa Trump Foundation - wanapaswa kupata mafunzo ya lazima kuhusu majukumu ya kuwa watendaji na wakurugenzi wa mifuko ya misaada", Mwanasheria Mkuu wa New York, Letitia James, alisema.

Kutokana na uamuzi huo wa mahakama, rais Trump, alitakiwa kukiri waziwazi juu ya matumizi mabaya ya fedha za mfuko huo na kueleza kwamba wakati mwingine atazingatia masharti ya matumizi ya fedha za mfuko huo.

Asasi ya kujitolea ya Donald Trump ilifungwa mwaka 2018 baada ya waendesha mashtaka kumshutumu kuwa anafanya kazi kidogo kuliko fedha zinazotumika.

Inadaiwa kuwa taasisi hiyo ya Trump na watoto wake watatu inapaswa kutohusishwa siasa, mahakama ilitoa uamuzi.

Vilevile suluhisho pekee la kesi hiyo ni kuwa lazima fedha hizo zilipwe na Trump mwenyewe.

"Trump anapaswa kulipa dola 2,000,000, kiasi ambacho kitaenda kwenye taasisi ya msaada kama bado ipo," aliandika jaji Saliann Scarpulla.

Alisema kuwa fedha hizo zinapaswa kwenda kwenye mifuko ya misaada minane ambayo Trump hana uhusiano nayo.

"Malipo ya fedha hizo ndio suluhisho la mwisho la kesi hiyo," alisema mwendesha mashtaka.

***BBC***

# HADITHI

# Jumba Jekundu-26

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**

Moyo ulikuwa unamuenda mbio, asijue afanye nini. Alijikuta akisimama kwenye mlango wa mbele wa yoyote aliyekuwa anaendesha gari hilo.

Taratibu kioo kilishuka chini kwa madaha. Ni kama vile aliona macho yake alimdanganya. "Ni yeye kweli?" Asema lakini si kwa sauti. "Pita upande wa pili upande ndani ya gari." Sauti ya aliyekuwa anaendesha gari ilimwambia kwa utulivu.

"Hakuna mtu mwingine ndani ya gari?" Kadili alijikuta akiropoka." Kicheko mwanana kilifuatia.

"Kadili umeanza kuwa mwoga siku hizi, hakuna mtu yoyote, njoo upande mara moja."

Kwa asilimia nyingi Kadili alimuamini dereva huyo. Hakuna mwingine ila ni Edina.

Alionekana kuendelea kuwa mrembo zaidi. Kadiri aliushangaa uzuri wa asili wa msichana huyo kwani kutokana na matatizo yote ambayo ameyasikia juu yake, kumtoroka mumewe, kukaa kusikojulikana na kufiwa na mama yake, bado hakuonekana kama amedhohofika au kusawijika kama alivyotarajia kuwa anaweza kuwa. Ndiyo kwanza aliendelea kunawiri wakati mwingine ni zaidi ya alivyokuwa akimuona miaka michache iliyopita 'Blue Hotel' walipokuwa akicheza disco.

"Umepajuaji hapa Edina." Lilikuwa ni swali la kwanza la Kadili baada ya kuketi kwenye gari.

Edina alirejea kicheko chake kama cha awali. "Hukumbuki kuwa ulishawahi kuniambia unaishi Tandale?"

"Unaitwa nani?"

"Kadili."

"Ok, unaishi wapi?"

"Naishi Tandale Kwa Tumbo."

"Nashukuru kukufahamu swahiba, mimi naitwa Edina, naishi Oysterbay."

Ndipo Kadili alipokumbuka kuwa walishawahi kuulizana majina na sehemu wanazoishi wakiwa wanajimwayamwaya kwenye disco kule Sinza.

"Kabla hatujaongea mengi Kadili, naomba kama kuna kitu ambacho unataka kwenda kufanya nyumbani nenda mara moja halafu urejee. Nadhani tuna maongezi marefu ambayo kwa hapa hatuwezi kuongea ndani ya gari. Inatakiwa kwende sehemu tulivu ambako hakutokuwa na watu wengi ili kujua na kuelezana kila kitu kilichotokea huko nyuma na tuwekane sana. Najua utakuwa na kinyongo moyoni mwako kutokana na yale uliyofanyiwa, lakini maongezi yanaweza kufanya tusameheane na kila mtu kurejea kwenye hali ya kawaida."




Edina aliongea kwa utulivu mkubwa.

Saa ilimuonyesha kuwa ni saa 10:00 jioni. Hakuna na kitu cha maana kilichokuwa kinamrejesha nyumbani zaidi ya uchovu tu.

"Hapana sina."

"Kwa hiyo tunaweza kwenda."

"Wapi?"

"Niamini Kadili, mimi ni rafiki na swahiba yako, siwezi kukupeleka sehemu yoyote yenye hatari, au nikahatarisha maisha yako. Na yote aliyokutokea, utajua ni nini yalitokea."

"Okay Edina twende."

Ndani ya gari kulikuwa kimya. Ni kama vile mtu na mateka wake. Inawezekana kila mmoja alikuwa akifikiria yale yaliyotokea huko nyuma na jinsi kila mmoja ataeleza nini kilitokea baada ya kuachana mpaka kutokea mambo ya kutekana, mateso, kukimbia mume na kifo cha Mama Pauline. Inawezekana kila mmoja alikuwa anataka wasaa wa kumuuliza mwenzake. Ndiyo maana walikuwa kimya kabisa.

Kadili alishindwa hata kumpa pole ya kufiwa na mama yake. Hakutaka kufanya haraka. Alitaka ajue kwanza mtazamo wake. Kikubwa tu ambacho alichokuwa anafikiria kwenye gari ni Edina anampeleka wapi?

Kingine ni kuomba Mungu asikutwe kwa watu ambao wanamfahamu mume wa Edina, kwani alikuwa na uhakika kuwa bado hajarejea kwa mumewe. Tangu alipomtoroka na kusababisha kifo cha mama yake mzazi Mama Pauline, alitaka kujua kama anaishi kwao kwenye jumba jekundu au sehemu nyingine.

Alichokuwa akiombea tu ni kwamba Edina asimpeleke kwao, kule ambako alikowahi kupelekwa na mabaunsa wakiongozwa na Mama Pauline, wakamsulubu kisawasawa kwa madai tu kuwa anamfuatafuata binti yao.

Gari haikuonekana kwenda Oysterbay. Badala yake ilipotoka Tandale ikapitia barabara ya Kijitonyama hadi maeneo ya Sayansi kwenye makutano na barabara ya Bagamoyo ikakata kushoto.

Ndani ya gari kulikuwa na gazeti. Kadili alichukua gazeti na kuanza kusoma. Hakutaka kumuuliza maswali Edina kwa sababu aliamini ni magumu, hivyo alihitaji wasaa na utulivu.

Ilipofika maeneo ya Tegeta, Edina alikata kulia na kuelekea maeneo ya Ununio. Mwisho wa gari ulikuwa kwenye hoteli moja mpya kabisa iitwayo Safari Beach.

"Tumefika." Aliongea Edina kwa utulivu.

Kadili hakujibu kitu. Aliteremka na kumfuata mwenyeji wake. Walipandisha ngazi hadi kwenye ghorofa ya nne, chumba namba 10.

Kilikuwa kimefungwa. Edina alifungua na kumkaribisha mgeni wake "Karibu ndani, usiwe na wasiwasi."

Kadili hakuona dhamira yoyote mbaya kwenye uso wa Edina tangu mwanzo. Hivyo wasiwasi kuhusu usalama wake ulifutika. Aliingia.

Kilikuwa ni chumba kikubwa chenye kila kitu kinachopatikana kwenye hoteli za kisasa.

Alijituma kwenye sofa laini. "Unakunywa nini mgeni wangu?" Akauliza kwa madaha.

"Juisi yoyote ile."

"Leo umekuwa mwanafunzi? Mbona wakati ule kule kwenye disco niliona kama wewe na rafiki yako mlikuwa mkinywa bia?"

"Bia huwa nakunywa kwa sababu maalum tu Edina, siyo muda wote wa kunywa pombe."

"Okay"

Alikwenda kwenye friji na kutoa boksi la juisi, pamoja na mrija, akamletea mgeni wake. Yeye mwenyewe mkononi alikuwa ameshika bia laini mkononi.

Kilipita kimya kama cha dakika mbili hivi, kila mmoja akionekana kutafakari cha kuanzia.

"Enhee lete stori." Edina aliovunja ukimya.

"Mimi hapa ni mgeni, kumbuka wewe ndiye uliyenitafuta, ukaja nyumbani unanichukua, nadhani wewe ndiyo utakuwa una cha kuniambia kwa nini umenileta hapa."

Edina aliguna, mguno uliotaka kuwa kama kicheko hivi.

"Sikutarajia kama Kadili unaongea hivi. Kumbe na wewe muongeaji eee? Kule tulipokuwa tunakutana kwenye disco ulikuwa unaongea kwa kifupi tu, ulionekana mpole sana, lakini leo naona umebadilika, au kule ulikuwa unaficha makucha?" Edina alimtania swahiba yake.

"Hapana, mwenye makucha ana makucha tu, hata kama akiyaficha anajulikana tu kama ana makucha. Mfano paka au simba, hata kama kificha makucha si utajua tu anayo."

Kicheko kilimtoka Edina. "Eee mwenzetu siku hizi umekuwa mwanafalsafa, hongera."

"Ahsante." Alikohoa kidogo na kuuliza.

"Hapa umekuja kwa muda mfupi au?"

"Niko hapa kwa miezi miwili sasa. Nimelipia kwa miezi mitatu kuishi hapa, bado mwezi mmoja pesa nililipia iishe."

Kadili hakutaka kujichosha sana kujua alipopata pesa ya kulipia hoteli ya kisasa kama hiyo kuishi kwa miezi mitatu kwa sababu Edina ni mtoto wa kitajiri.

"Si nilisikia umeolewa mumeo yuko wapi?"

"Ulisikia wapi?"

"Kwani siri Edina? Mimi mwenyewe niliona kwenye gazeti umefunga ndoa ya Dk. Deus Kapilima na picha kabisa umepiga na mumeo."

Edina alinyamaza kidogo, akanywa funda kadhaa za bia yake akaiweka kwenye meza.

"Ni hadithi ndefu sana Kadili." Sasa aliongea kwa utulivu na hisia.

"Sijui nianzie wapi?"

"Mimi nakuomba uanzie wakati ule tulipokuwa tunakutana kule disco. Mara ukatuambia kuwa umepigwa marufuku kuja 'blue star'. Baadaye wakaja kunikamata mimi sijui wale jamaa mabausa walipajuaje nyumbani? Nadhani hapo ndipo anzia.

"Kadili unakumbuka wakati ule nilipokuuliza kuwa unaishi wapi ukaniambia Tandale?"

"Ndiyo?"

"Kuna mlinzi mmoja alisikia, ndiyo aliyesema nyumbani kuwa unaishi Tandale, nadhani swali lako nitakuwa nimekujibu." Alisema na kuongeza.

"Kwa ufupi ni kwamba mama yangu mzazi ambaye kwa sasa ni marehemu kwa muda mrefu alikuwa anataka mimi niolewe. Tena niolewe na wanaume ambao anawafahamu yeye na si mimi. Alikuwa listi ya wanaume ambao ni matajiri, wafanyabiashara wakubwa, madaktari bingwa, wanasiasa, na mastaa wengi, lakini mimi nilikataa kwa sababu sikuwa nashirikishwa. Huwezi kuolewa na mtu ambaye humpendi, au umeletewa tu, hamfahamiani."

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

## NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

## MCHANGANYIKO

**KISIMA CHA BEI NAFUU KILICHOKAMILIKA:** Tutakuchimbia kisima na kukuwekea pampu, tutaacha maji yanatoka kisimani kwako. tupigie Simu:0714 564 651 / 0692 006 546.


**Tunasafifisha visima virefu na vifupi** kwa kumia mashineza kisasa na tunapima ubora wa maji.Gharama zetu nafuu!! Simu:0623 528 465 / 0657 746 365.

**Kuchimba kisima Dar na Pwani** kwa gharama nafuu!! Mita 1 Sh.60,000/= tu! Tunaweka bomba (UPVC), kokoto (Gravels) na pampu bure! Piga:0623 528 465 / 0657 746 365.

## 2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

## CHETI KIMEPOTEA



**LEONARD JOSEPH** anatangaza kupotelewa na cheti cha KIDATO CHA NNE chenye no **S3017-0042** kilichotolewa na NECTA TANZANIA mwaka 2014.. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/443945/2019**

115509902


## KUPOTEA KWA VYETI



**Josephina Charles** Ismail anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0307-0047** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika Shule ya Sekondari Central . Cheti cha chuo kilichotolewa na Chuo cha Local Government Training Institute mwaka 2014. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MBI/RB/474/2019**

115509102

## KUPOTEA KWA HATI YA MATOKEO(RESULT SLIP)



**Nyanda Charles Nyanda** anatangaza kupotea kwa hati ya Matokeo (RESULT SLIP) yenye index namba **S1375/0637** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika S hule ya Sekondari New Era. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/BUE/RB/454082/2019**

115509202

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**Rodgers Arnold Munisi** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA DELTA** yenye namba za usajili **T 570 DFP** Chassis No. **SCP921014402** Engine No. **2521546637** Yenye rangi NYEKUNDU. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/454080/2019**

115509502

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO.LTD** kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC** tutauza dhamana ya **STEWART E. MWANGALABA** Gari namba T 181 DMF Toyota RAV 4 New Model,Black Metalic. Mnada utafanyika Dsm- Magomeni Mikumi/Lango la Jiji.

Mnada utafanyika tarehe 02/12/2019, mteja atatakiwa kulipa 25% siku yam nada na 75% ilipwe ndani ya siku tatu (3) ukishindwa utakuwa umepoteza malipo ya awali 25%. Pia Gharama za kubadilisha umiliki zitakuwa ni juu ya mnunuzi wa Gari.

**MAWASILIANO YETU:-**
**TAUSI AUCTION MART 0719 351 040**
**NA AKIBA BANK – 0719 922 700.**

115508602


## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD HARUNY MWALONGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5105-0053** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **UMAWANJO SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/437713/2019.**

115508202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Geophrey Edwine Mwakibete** anatangaza kupotea kwa Cheti cha Certificate in East African Customs Clearing, and Freight Forward Practice chenye namba ISO **9001:2008** kilichotolewa na Chuo cha Institute Of Tax Administration mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/URA/RB/451510/2019**

115508802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Distributed via ippmedia

**SULEIMAN HANZURUNI MVUNYE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya HARRIER yenye namba za usajili **T 849 CLP** Chassis namba **SXU100001100** Engine na. **5S0705451** range Black. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOD/TR/454951/2019**

215507802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA:288/2019.**

**JOSEPHINA LUDOVICK................. MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PAULINA PAUL ..................... MJIBU MAOMBI**

**KWA: PAULINA PAUL**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 288/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 11.11.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi. Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 05.11.2019

115509802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILLIAM SILLA URONU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 369 DCY TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/455210/2019.**

115510402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO. 114 LA 2019**

**SASA GROUP LIMITED.....................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MOKHA AGANEY CO LIMITED.......MJIBU MAOMBI WA KWANZA**

**DYAMIC FREIGHTS FORWADERS.........MJIBU MAOMBI WA PILI**

**MOHAMED RASHID LEMA................MJIBU MAOMBI WA TATU**

**JOHN JACOB GAP...........................MJIBU MAOMBI WA NNE**

**KWA: JOHN JACOB GAPI**
**C/O MANAGING DIRECTOR**
**MOKHA AGENCY CO. LIMITED**
**USHIRIKA TOWER, LUMUMBA STREET,**
**P.O. Box 1664**
**DAR ES SALAAM**
**Mob. 0677000111**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri la aridhi dhidi yako unatakiwa kufika katika Mahakama hii tukufu wewe mwenyewe au wakili wako au mwakilishi wako anayetambuliwa kisheria tarehe 11/11/2019 saa 9:00 asubuhi mbele ya **Mh. J. MASABO** ili kujibu madai dhidi yako.

Unaagizwa kuleta vielelezo vyote hapo juu ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**KUMBUKA:** Kuwa usipohudhuria siku hiyo, na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito huu, shauri hili litasikilizwa na kutolewa maamuzi bila wewe mwenyewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 10. 2019.

115509702

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**JESCA BENJAMINI KOMBA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1144/0641** iliyotolewa na ISIMILA SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/SEL/RB/455069/2019.**

115509302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LATINES NOA LEKENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **COROLLA** yenye namba za usajili **724 ATX** Chassis namba **AE913187687 Engine na. AE2900278.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/263593/2019**

115510002

## TWINS DAY/ MAPACHA DAY – 11/11/

**EDEN WOMEN GROUP – KIKUNDI CHA AKINA MAMA EDEN** wanawakaribisha kuja kusherehekea TWINS DAY itakayofanyika ndani ya **EDEN CENTRE MISUFINI KIBAHA** kuanzia saa 6 hadi saa 9 mchana. Leta watoto mapacha wapate zawadi siku hiyo na michezo kwa watoto wote.

**Mawasiliano: JOY DANIEL 0767562452 au HOSSANA DANIEL 0657 382803. WOTE MNAKARIBISHWA.**

115510402

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# NEYMAR

## AJIANDAA KURUDI DIMBANI

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR atarudi kwenye mazoezi na kikosi cha Paris Saint-Germain wiki ijayo, lakini mchezaji mwenzake, Mauro Icardi anahitaji kuwa fiti kwa mchezo wa leo Jumamosi wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Brest.

Mshambuliaji huyo wa Brazil hajaichezea PSG tangu iliposhinda 4-0 dhidi ya Angers Oktoba 5 mwaka huu baada ya kuumia misuli ya paja kwenye mechi za kimataifa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ameanza kufanya mazoezi binafsi na atajihakikishia kupona wiki ijayo, akiwa ameachwa kwenye kikosi cha Brazil katika mechi za kirafiki mwezi huu.

PSG pengine inaweza kuwa bila Icardi katika mchezo wake wa ligi, ingawa mshambuliaji huyo anayecheza kwa mkopo hapo akitokea Inter alitolewa kipindi cha pili kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa iliyochezwa Jumatano wakati wakishinda bao 1-0 dhidi ya Club Brugge.

Kocha, Thomas Tuchel alisema baada ya mchezo huo kuwa, Icardi amekuwa akicheza huku akiwa na maumivu, na jana Ijumaa angefanyiwa tathimini zaidi.

Thilo Kehrer amerudi kwenye mazoezi kwa ajili ya kuivaa Brest, lakini Ander Herrera atakuwa nje ya uwanja kwa sababu ya maumivu ya paja, huku Thomas Meunier pia atakuwa nje hadi baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Mabingwa PSG walifungwa 2-1 na Dijon wikiendi iliyopita, lakini wanaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi saba dhidi ya Angers waliopo nafasi ya pili.

## DESCHAMPS: GRIEZMANN ATANG'ARA ZAIDI BARCELONA

**PARIS, Ufaransa**

ANTOINE Griezmann atafurahia mafanikio zaidi kwa kipindi chake akicheza Barcelona, kwa mujibu wa Didier Deschamps.

Griezmann aliondoka Atletico Madrid kwenda Barca kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 120 kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini hajawa kwenye kiwango chake hadi sasa pale kwenye dimba la Camp Nou.

Akiwa amecheza zaidi kama mshambuliaji wa kati kwenye kikosi cha Ufaransa na Atletico, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amefunga mabao manne kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, katika mechi 10 alizocheza.

Hata hivyo, Deschamps haoni tatizo kwa Griezmann, huku akidai kwamba anahitaji muda zaidi kuzoea maisha kwenye klabu yake mpya.

"Sina shaka nae. Hata kama unakuwa na wachezaji wakubwa pale Barcelona, haitokei tu siku moja. Inategemea na namna gani unacheza," amesema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari baada ya kumchagua Griezmann kwenye kikosi cha Ufaransa kwa ajili ya mechi za kimataifa.

"Pia anaonyesha tofauti, anacheza nafasi tofauti na akiwa kikosi cha Ufaransa, ingawa anacheza kwa kujiachia zaidi."




## SOKRATIS: SIJALI NANI NAHODHA ARSENAL

**LONDON, England**

MCHEZAJI Sokratis Papastathopoulos amesisitiza hajali nani anavaa kitambaa cha unahodha pale Arsenal baada ya Granit Xhaka kuvuliwa na kupewa Pierre-Emerick Aubameyang.


Kocha Unai Emery alitangaza Jumanne kwamba, Xhaka amevuliwa kitambaa cha unahodha baada ya kukwaruzana na mashabiki wakati wa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace.

Aubameyang atachukua uongozi wa klabu hiyo, akianzia leo Jumamosi kwenye mchezo dhidi ya Leicester City, lakini Sokratis anaona kwamba hakuna tatizo lolote ilimradi mambo yanakwenda sawa uwanjani.

"Nafikiri ni mara yake ya kwanza anakuwa nahodha," alisema Sokratis kwa mujibu wa magazeti ya Uingereza.

"Kwangu mimi jambo la kwanza Aubameyang anatakiwa kufanya ni kufunga, anatakiwa kufanya kazi yake. Unahodha sio kitu muhimu, tunachoangalia kwanza ni umuhimu wake uwanjani.

"Ni mtu mzuri, lakini nani anakuwa nahodha hilo sio jambo muhimu kwetu. Jambo la msingi ni kwamba timu yote iko vizuri na tunapata ushindi uwanjani. Sisi ni kama familia. Mwishoni tunatakiwa kuwa na matokeo mazuri uwanjani."



## HABARI MICHEZO



# KUMBE WENGER ALIOMBA KUWA KOCHA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

JARIDA la michezo la Bild la nchini Ujerumani, limefichua siri ya mazungumzo yaliyokua yakiendelea kati ya uongozi wa mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich na aliyekuwa kocha wa Arsenal, Arsene Wenger.

Jarida hilo limeeleza kuwa, Wenger alianza mawasiliano na uongozi wa Bayern Munich kwa ajili ya kuomba nafasi ya kuwa kocha, kutokana na mwenendo mbaya wa kocha aliyefukuzwa klabuni hapo, Niko Kovac.

Mfaransa huyo aliwasilisha ombi lake kwa mwenyekiti wa klabu hiyo, Karl-Heinz Rummenigge, baada ya matokeo mabaya waliyopata Bavaria hao mwishoni mwa juma lililopita dhidi ya Eintracht Frankfurt, walioibuka na ushindi wa mabao 5-1.

"Arsene Wenger alimpigia simu Karl-Heinz Rummenigge Jumatano, kwa nia ya kumwomba nafasi ya kuwa kocha mkuu wa kikosi, kufuatia fununu za kutaka kutimuliwa kwa Kovac," limeeleza jarida la Bild.

Uongozi wa Bayern Munich umekiri kufurahishwa na uwezo wa Wenger tangu alipokua na kikosi cha Arsenal ya England, lakini umesisitiza kutokua tayari kufanya naye kazi kama kocha mkuu wa kikosi chao.

Kocha Hansi Flick ambaye alikua msaidizi wa Joachim Low kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Ujerumani, anapewa nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Nico Kovac.

Distributed via ippmedia

# Solskjaer ahofia kumkosa McTominay



**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amethibitisha kwamba, Scott McTominay aliumia kifundo cha mguu wakati Manchester United ikipata ushindi dhidi ya Partizan Belgrade, huku akionyesha kutokuwa na hofu kuhusu hali ya Harry Maguire.

United ilipata ushindi wa mabao 3-0 juzi Alhamisi kwenye Ligi ya Europa, shukrani kwa mabao ya Mason Greenwood, Anthony Martial na Marcus Rashford.

McTominay alitolewa nje kipindi cha pili, huku pia kukiwa na hofu juu ya ufiti wa Maguire.

Lakini wakati kukiwa na hofu ndogo juu ya hali ya afya ya Maguire, kocha wa United, Solskjaer amethibitisha kuhusu hali ya McTominay.

"Nafikiri Harry atakuwa fiti. Alimaliza mchezo," alisema akiiambia televisheni ya MUTV.

"Scott ndio haswa anaonekana ana tatizo, ngoja tunaangalia wiki chache zijazo.

"Alisema atakuwa fiti nje ya uwanja na alisema atakuwa poa. Atakuwa na wakati mzuri kurudi uwanjani.

"Nafikiri atakuwa fiti kabla ya Jumapili, lakini sijui. Ndani ya kifundo chake cha mguu. Nafikiri atakuwa fiti na atakuwa amepona kifundo cha mguu."

Wakiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, United kesho itakutana na Brighton and Hove Albion.

Ushindi dhidi ya Partizan umewapa hamasa vijana wa Solskjaer ili kurudi kwenye kiwango chake kwenye Ligi Kuu, huku ikijumuisha washambuliaji vijana kama vile Greenwood, Rashford na Martial.

"Sababu ya kuwachezesha wote watatu pamoja ni kwamba tunajua wanakuwa hatari, tukiwa na wachezaji hao tunakuwa na nafasi nzuri ya kutengeneza nafasi ya kufunga," amesema.

"Alifanya vizuri, na mtu makini kwenye kumalizia. Alitulia na kumsubiri golikipa. Bao la pili lilitoka kwa Anthony na pengine lilikuwa bora zaidi usiku ule.

"Halafu tukatapa bao la Marcus ambaye alimalizia kwa mguu wake wa kushoto. Atapata nafasi hizo kila wakati."

# Son ampa mabao yake Gomes

**LONDON, England**

NYOTA wa klabu ya Tottenham Spurs, Heung-min Son ameonyesha uungwana Jumatano katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufunga mabao mawili dhidi ya Red Star Belgrade na kuzisogelea kamera na kuonyesha ishara ya kumwomba msamaha, Andre Gomes.

Mabao hayo, Son aliyafunga katika mchezo ambao Tottenham iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Red Star Belgrade kwenye Uwanja wa Rajko Mitic.

Mkorea huyo, alisema hakutaka kushangilia kama sehemu ya kusikitishwa na kile kilichotokea kwa bahati mbaya kati yake na Gomes katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu England alipomuumiza vibaya bila ya kutegemea.

"Namtakiwa Andre Gomes apone haraka," alisema nyota huyo, akizungumzia tukio hilo kwa mara ya kwanza tangu litokee siku chache zilizopita.

"Nimekuwa na siku ngumu, kiukweli zilikuwa ngumu haswa, lakini kila mmoja amekuwa akinitumia meseji na kutaka niwe jasiri kukubaliana na kilichotokea, nachoweza kusema ni samahani kwa kilichotokea," alisema Son.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOUTHGATE AMWITA MADDISON ENGLAND

***Ni kwa ajili ya maandalizi ya mechi za kusaka tiketi ya Euro 2020 dhidi ya Montenegro, Kosovo...

**LONDON, England**

KIUNGO wa klabu ya Leicester City, James Maddison, ametajwa katika kikosi cha timu ya taifa ya England, ambacho mwanzoni mwa juma lijalo kitaanza maandalizi ya michezo ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Ulaya (Euro 2020).

England watakuwa wenyeji wa Montenegro Novemba 14 mwaka huu na siku tatu baadaye watapapatuana na Kosovo.

Kocha wa England, Gareth Southgate amemtaja Maddison, kwenye kikosi chake, licha ya kukabiliwa na skendo za kupigwa picha akiwa katika Casino, baada ya kuondolewa kikosini mwezi uliopia kwa sababu za kuwa majeruhi.

Kiungo huyo tayari ameshaitwa kwenye kikosi cha England mara tatu, lakini hajafanikiwa kucheza mchezo hata mmoja.

Southgate amesema anaendelea kutambua mchango wa Maddison na ndio maana anaonyesha kumwamini kwa kumuita kwenye kikosi cha timu hiyo, na daima hatoyapa nafasi mambo yaliyowahi kuzungumzwa na vyombo vya habari kuhusu maisha yake binafsi.

"Ninaendelea kupendezwa na uwezo wake anapokua uwanjani, nimedhihirisha hilo kwa kumwita kwa mara ya tatu sasa, japo hajawahi kucheza," alisema Southgate.

"Mara ya mwisho nilipanga kumtumia katika kikosi changu lakini kwa bahati mbaya alipatwa na majeraha."

"Najua baadhi yenu mtakuwa mmeshangazwa na hatua ya kumuitwa kwenye kikosi kwa kukumbuka tukio lililoandikwa katika vyombo vya habari, binafsi siangalii maisha binafsi ya mchezaji anapokua nje ya soka, hata kama alikua mgonjwa, suala la kuonekana Casino ilikua ni kupenda kwake."

Kwa upande mwingine kocha huyo amemwita beki John Stones, kiungo Alex Oxlade-Chamberlain na mshambuliaji wa pembeni, Callum Hudson-Odoi.

England inaongoza msimamo wa Kundi A, na kuelekea michezo ya mwezi huu inahitaji alama moja ili ifuzu fainali michuano hiyo ya Ulaya (Euro 2020).

Kikosi kamili.

Makipa: Tom Heaton (Aston Villa), Jordan Pickford (Everton) na Nick Pope (Burnley) Mabeki: Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Ben Chilwell (Leicester), Joe Gomez (Liverpool), Harry Maguire (Manchester United), Tyrone Mings (Aston Villa), Danny Rose (Tottenham), John Stones (Manchester City), Fikayo Tomori (Chelsea) na Kieran Trippier (Atletico Madrid)

Viungo: Ross Barkley (Chelsea), Fabian Delph (Everton), Jordan Henderson (Liverpool), James Maddison (Leicester City), Mason Mount (Chelsea), Alex Oxlade-Chamberlain (Liverpool), Declan Rice (West Ham) na Harry Winks (Tottenham)

Washambuliaji: Tammy Abraham (Chelsea), Callum Hudson-Odoi (Chelsea), Harry Kane (Tottenham), Marcus Rashford (Manchester United), Jadon Sancho (Borussia Dortmund), Raheem Sterling (Manchester City) na Callum Wilson (Bournemouth).

## KWA UFUPI

### XHAKA ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United iko tayari kumsajili kiungo wa Arsenal na raia wa Uswiswi, Granit Xhaka (27), ambaye anatarajia kuondoka katika klabu yake katika dirisha dogo la Januari. ***(Times - subscription required)***

### AUBAMEYANG ANUKIA BARCA
BARCELONA imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Gabon na Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (30). Vigogo hao wa Hispania wanatarajia kuwasilisha ofa ya kumnunua mchezaji huyo mapema Januari. ***(El Chiringuito via Mirror)***

### ARSENAL, TORREIRA KUTETA
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Lucas Torreira, ambaye ana umri wa miaka 23, anajiandaa kufanya mazungumzo na mabosi wa Arsenal kwa ajili ya kujadili hatima yake. ***(Mirror)***

### ZLATAN KUREJEA MILAN
ZLATAN Ibrahimovi anajiandaa kurejea katika klabu ya AC Milan. Straika huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Sweden ambaye ana umri wa miaka 38 kwa sasa anatarajia kumaliza mkataba wa kuitumikia LA Galaxy ya Marekani. ***(ESPN, via Calciomercato)***

### HAALAND KUTUA LEIPZIG
STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (19), huenda akazikacha ofa za kujiunga na Manchester United, Liverpool pamoja na Arsenal na kuamua kuelekea RB Leipzig inayoshiriki Ligi ya Bundesliga akitokea Red Bull Salzburg katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Sky Sports)***

### GUARDIOLA ATAJWA ITALIA
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ambaye mkataba wake na klabu hiyo unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu ujao, atakuwa huru kujiunga na kikosi cha Italia endapo mabingwa hao wa Ligi Kuu England wataamua kuachana naye. ***(Times - subscription required)***

### MCNEIL AJIPANGA EPL
WINGA wa Burnley na Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21, Dwight McNeil (19), amesema kuwa kwa sasa anajipanga zaidi kuimarisha kiwango chake na kuliko kufikiria tetesi za kuwaniwa na Manchester United. ***(Mirror)***

### RODIGUEZ AGOMBEWA
MANCHESTER United, Tottenham na Wolves zote kwa pamoja zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), kutoka Real Madrid katika dirisha dogo la Januari. ***(El Desmarque - in Spanish)***

### WEGHORST ANUKIA PALACE
CRYSTAL Palace inaendelea na mchakato wa kuangalia kiwango cha straika wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Wout Weghorst (27), ambaye ameshafunga mabao nane katika mechi 15 alizoichezea Wolfsburg msimu huu. ***(Calciomercato - in Italian)***

### ARSENAL, WEST VITANI
ARSENAL itapambana na West Ham katika vita ya kuwania saini ya beki wa Timu ya Taifa ya Austria, Martin Hinteregger (27), anayeichezea Eintracht Frankfurt. Imeelezwa kuwa thamani ya nyota huyo ni pauni milioni 22. ***(Sun)***

### GRANT ANG'ARA SOKONI
KLABU ya Bournemouth na Wolves zimeweka wazi nia yao ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Huddersfield, Karlan Grant (20) katika kipindi cha usajili cha dirisha dogo hapo Januari. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

# STARS YASOGEZA MBELE CHALENJI YA WANAWAKE

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji yamesogezwa mbele kwa muda wa siku mbili ili kupisha maandalizi ya mchezo wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021), kati ya wenyeji Timu ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya Equatorila Guinea, imefahamika.

Taifa Stars inatarajia kuikaribisha Equatorial Guinea Novemba 15 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, alisema kuwa michuano hiyo ambayo itashirikisha nchi 10, sasa itafanyika kuanzia Novemba 16 hadi 25 mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini.

Musonye alisema wameona si busara kuanza michuano hiyo, wakati wenyeji wanahitaji kujiandaa vema dhidi ya mchezo huo wa kimataifa na wanaamini, muda ulioongezeka, utazisaidia timu kuendelea kujiimarisha zaidi.

"Sasa mashindano yataanza Novemba 16, hii ni kwa sababu ya mechi kati ya Tanzania na Equatorial Guinea, mechi zote ni muhimu katika maendeleo ya soka kwenye ukanda wetu," alisema Musonye.

Alisema kuwa mechi ya ufunguzi katika mashindano hayo itakuwa kati ya wenyeji, Timu ya Taifa ya Tanzania Bara maarufu Kilimanjaro Queens dhidi ya Sudan Kusini itakayochezwa kuanzia saa 10:30 jioni, wakati mapema mchana Burundi wataivaa Zanzibar Queens.

Alieleza kuwa timu zinazoshiriki mashindano hayo zimepangwa katika makundi mawili, Kundi A likiwa na wenyeji Kilimanjaro Queens, Zanzibar Queens, Sudan Kusini na Burundi wakati Ethiopia, Kenya, Uganda na Djibouti wako Kundi B.

Aliongeza kuwa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) ndiyo linasaidia gharama za kuendesha mashindano hayo ya wanawake pamoja na michuano ya vijana ya umri chini ya miaka 15 (U-15) na (U-20).

Kilimanjaro Queens inayonolewa na Bakari Shime "Mchawi Mweusi" inashikilia ubingwa wa mashindano hayo mara mbili mfululizo, baada ya kushinda taji hilo mwaka 2016 mjini Jinja, Uganda na mwaka jana yalipofanyika kwenye Uwanja wa Nyamirambo jijini Kigali, Rwanda.




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akidhibitiwa na beki wa Tanzania Prisons, Nurdin Chona (aliyeanguka), katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Prisons alia na mastraika

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Adolph Rishard, amesema kuwa kikosi chake kina tatizo la umaliziaji na kama si hivyo, wangeibuka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba ambayo ilichezwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ilimalizika kwa sare ya bila kufungana, lakini Tanzania Prisons, ikiendelea kushikilia rekodi ya kutopoteza mchezo hata mmoja tangu msimu huu ulipoanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rishard, alisema kuwa kama wachezaji wake wangeongeza umakini zaidi, wangepata ushindi katika mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani katika dakika zote 90.

Kocha huyo alikiri pia Simba ina kikosi imara, chenye wachezaji wazoefu na kama si ubora wao, wangeondoka na pointi tatu.

"Simba ni timu nzuri, katika timu zote tulizocheza, leo (juzi) ndio tumepata wakati mgumu, ndio maana tulikuwa tunacheza kwa kuvizia," alisema kocha huyo.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza vema katika mchezo huo uliokuwa na ushindani, lakini akaweka wazi kwamba ataendelea kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

"Katika kipindi cha kwanza tulitengeneza nafasi tatu, na katika kipindi cha pili tulitengeneza nafasi mbili, hii ni taswira nzuri kuwa wanafuata maelekezo, ila pointi moja tuliyopata si mbaya, itatusaidia," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi za jana, Ligi Kuu Tanzania Bara inasimama kwa muda kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inatarajia kuikaribisha Equatorial Guinea Novemba 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa na baadaye kuikabili Libya ugenini, siku nne baadaye.

## MSIMAMO LIGI KUU

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 9 | 7 | 1 | 1 | 16 | 3 | 22 |
| 2. Lipuli | 10 | 5 | 3 | 2 | 18 | 10 | 18 |
| 3. Kagera Sugar | 9 | 5 | 2 | 2 | 12 | 7 | 17 |
| 4. Tanzania Prisons | 10 | 4 | 6 | 0 | 12 | 8 | 16 |
| 5. Namungo | 10 | 4 | 1 | 4 | 8 | 7 | 16 |
| 6. JKT Tanzania | 10 | 4 | 3 | 3 | 7 | 7 | 15 |
| 7. Mtibwa Sugar | 11 | 4 | 3 | 4 | 10 | 11 | 15 |
| 8. Ruvu Shooting | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 9. Alliance | 10 | 3 | 5 | 2 | 8 | 7 | 14 |
| 10. Mbao | 11 | 3 | 5 | 3 | 9 | 10 | 14 |
| 11. Polisi Tanzania | 9 | 4 | 1 | 4 | 9 | 10 | 13 |
| 12. Coastal Union | 10 | 3 | 2 | 5 | 8 | 9 | 11 |
| 13. Mwadui | 11 | 2 | 5 | 4 | 7 | 10 | 11 |
| 14. Azam | 6 | 3 | 2 | 2 | 5 | 3 | 10 |
| 15. Kinondoni MC | 7 | 2 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 |
| 16. Biashara United | 9 | 2 | 2 | 5 | 5 | 9 | 8 |
| 17. Mbeya City | 10 | 1 | 5 | 4 | 7 | 16 | 8 |
| 18. Young Africans | 4 | 2 | 1 | 1 | 5 | 4 | 7 |
| 19. Ndanda | 8 | 1 | 4 | 3 | 6 | 8 | 7 |
| 20. Singida United | 10 | 0 | 4 | 6 | 4 | 15 | 4 |

# Michuano gofu kufanyika Arusha

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Gofu Tanzania (TGU), kimesema kuwa mashindano ya wazi ya mchezo huo yamepangwa kufanyika kuanzia Novemba 29 hadi Desemba Mosi mwaka huu kwenye viwanja vya Kili Golf Wildlife jijini Arusha.

Shindano hili ambalo ni mahsusi kwa wachezaji wa Kundi A wenye "handicap kuanzia 0 hadi 9, limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya TGU na Taasisi ya Verge Africa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa TGU, Chris Martin, alisema kuwa maandalizi ya mashindano hayo yako katika hatua za mwisho na chama kinatarajia michuano hiyo kuwa na ushindani zaidi.

Martin alisema kuwa katika wachezaji wa Kundi A wenye "handicap 0 hadi 9 yatashirikishwa pia makundi mengine matatu ambayo ni Kundi B la wachezaji wanaume wenye "handicap 10 hadi 18 na lingine la Wazee "Senior players" wenye umri kuanzia miaka 6.

Alisema kuwa wapo wachezaji watakaoshiriki ambao wana handicap 10 hadi 18 na wachezaji wa kulipwa.

"Kundi A litacheza mashimo 72 kwa siku 3 na makundi mengine yanayoshirikishwa yatacheza katika mashimo 36 tu kwa siku mbili. Mshindi kwa Kundi A atapatikana kutokana na idadi ya jumla ya mikwaju atakayocheza mchezaji katika mashimo 72. Kwa makundi mengine mshindi atapatikana kwa "Net score" kutokana na mashimo 36," alisema Martin.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa hakuna mchezaji atakayeruhusiwa kucheza zaidi ya handicap 18 na usajili wa wachezaji wanaotarajiwa kushiriki ufungwa Novemba 22, mwaka huu.

Aliwataka wachezaji wote wa hapa nchini kujisajili kupitia katika klabu zao huku wale wa kimataifa kuwasiliana na chama ili kufahamu taratibu za kujiandikisha.

# Michezo

Jumamosi Novemba 9, 2019

Nipashe




## Southgate amwita Maddison England

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Kagera Sugar, Yusuph Muhilu (kushoto), akiwatoka wachezaji wa KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Kagera Sugar ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YAFANYA KWELI LIGI KUU

●●● Yaifunga Ndanda bao 1-0 ndani ya Nangwanda, lakini gonjwa la Zahera lamtesa Mkwasa...

**Na Isaac Kijoti, MTWARA**

MRITHI wa Mwinyi Zahera, Boniface Mkwasa "Master", ameanza kazi yake vema ya kuiongoza Yanga baada ya kuwafurahisha mashabiki na wanachama wa timu hiyo kwa kuipa ushindi dhidi ya wenyeji Ndanda FC jana.

Katika mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini hapa, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0, shukrani zikimwendea Mnyarwanda Patrick Sibomana aliyezamisha kimyani mpira wa faulo dakika ya 75.

Huo ni ushindi wa tatu kwa Yanga msimu huu na wa kwanza kwa Mkwasa tangu alipokabidhiwa mikoba ya kuinoa timu hiyo Jumanne wiki hii baada ya 'ndoa ya Zahera na klabu hiyo' kuvunjika.

Aidha, ushindi huo unaifanya Yanga kufikisha pointi 10 baada ya kushuka dimbani mara tano ikipoteza mchezo mmoja na kutoka sare moja.

Hata hivyo, gonjwa la safu ya ushambuliaji kukosa umakini tangu ikiwa chini ya Zahera kwa kutegemea kupata mabao kwa kutumia mipira iliyokufa ndilo lililoonekana kumtesa Mkwasa na sasa itabidi kulifanyia kazi.

Katika kipindi cha kwanza licha ya Yanga kumiliki mpira kwa asilimia kubwa haikuweza kutumia vema nafasi ilizotengeneza katika mchezo huo, tatizo likionekana kuwa lile lile la safu ya ushambuliaji kukosa umakini na hivyo kushindwa kutumia vizuri nafasi mbalimbali inazotengeneza na kuwapa presha mashabiki wao.

Pamoja na hali ya Uwanja wa Nangwanda kutokuwa rafiki, lakini kama Yanga ingekuwa makini kwa faulo ya dakika ya 33 iliyopigwa na David Molinga, mambo yangeweza kuwa tofauti. Kadhalika, Molinga alichezewa faulo na Samweli Mahulo dakika ya 43 lakini safari hii Juma Abdul alishindwa kuitendea haki na Yanga kukosa bao.

Kwa ujumla kucheza kwa nidhamu na umakini kwa mabeki wa Ndanda huku Yanga ugonjwa wao wa kutokuwa watulivu katika safu ya ushambuliaji ndilo lililoendelea kuwa tatizo la kukosa mabao kipindi cha kwanza.

Lakini pia tatizo la Ndanda kulinda zaidi huku wakishindwa kucheza kwa mashambulizi ya kushtukiza kuliwaacha huru zaidi mabeki wa Yanga na kuruhusu mashambulizi kwao ambayo hayakuwa na madhara kutokana na ubutu wa safu ya ushambuliaji wa wapinzani wao.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi huku Ndanda ikijilinda zaidi na kusababisha mashambulizi mengi langoni mwao huku Deus Kaseke akionekana kuwa mwiba mkali kwao, lakini madhara yake makubwa yalikuwa dakika ya 51 ambapo shuti lake litoka nje.

Dakika ya 59, Sibomana alishindwa kuwa makini kulenga lango baada ya kushindwa kuitendea haki krosi ya Kaseke lakini kuingia kwa Mrisho Ngassa dakika ya 64 akichukua nafasi ya Rafael Daudi kulizaa matokeo chanya baada ya kufanyiwa faulo dakika ya 74 iliyopigwa na Molinga kabla ya mwamuzi kuamuru irudiwe na safari hii ikipigwa na Sibomana aliyefunga bao na kuifanya timu hiyo ipate pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

Licha ya Ndanda kuhaha ikitaka kusawazisha safu ya ulinzi ya Yanga ikiwa chini ya Kelvin Yondani ilikuwa makini huku kiungo cha kati kikiifanya kazi yake vema kwa kukabia kati.

## Aussems akubali Prisons wanajua

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kushindwa kutamba, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi cha Tanzania Prisons ni imara na kimempa ushindani wa hali ya juu katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliowakutanisha kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Aussems, alikisifia kikosi cha Prisons kwa kuonyesha soka safi na kwamba ni mara yake ya kwanza kukutana na timu iliyojipanga vema.

Aussems alisema kuwa wapinzani wao walifanikiwa kuwabana na hivyo, nyota wake walishindwa kufanya mashambulizi kila walivyokuwa wanajipanga kuelekea kwenye lao la Prisons, hali iliyopelekea mchezo huo kumalizika kwa sare ya bila kufungana.

Alisema pia hakushangazwa na kiwango na Prisons, kwa sababu ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mchezo hata mmoja tangu msimu huu ulipoanza.

"Tangu nimekuja Tanzania, hii ni mara ya kwanza kuona timu iliyojipanga kama hii, walikuja hapa kwa ajili ya kupunguza nafasi, walikuja kwa lengo la kujilinda, walijilinda vizuri, nawapongeza kwa hilo," alisema Aussems.

Naye nahodha msaidizi wa Simba, Erasto Nyoni, alisema kuwa mechi hiyo ilikuwa na ushindani na siku hiyo ya juzi, timu yao haikuwa na bahati.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, kwetu na kwao pia, tuliingia na mbinu zetu, lakini tulishindwa kupenya, tulipambana, tulitumia njia mbalimbali kuhakikisha tunafika golini, lakini hatukuweza kupata bao," alisema beki huyo.

Baada ya kumalizika kwa majukumu ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inakabiliwa na mechi mbili za kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021), Simba itakutana na Ruvu Shooting katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Mabingwa hao watetezi, Simba ambao wamecheza mechi tisa ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 22, wakati Singida United yenye pointi nne lakini imeshuka dimbani mara 10, inaburuza mkia.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >